

Kongamano la kwanza la uwekezaji halal Tanzania

■ Wakati Tanzania ikilenga uchumi wa dola trilioni moja ifikapo 2050, Shirkah Invest imeandaa Tanzania Halal Investment Summit, kongamano litakaloibua fursa za mitaji na uwekezaji unaozingatia misingi ya Sharia.



■ CIFCA na Taqseem Academy watia nguvu




The Islamic Foundation, TAMSIA wajipanga kushirikiana



Wafanyabiashara wapewa misingi sita ya kufanya biashara ya halal

Wataalamu waenzi mchango wa Waqf, wataka mageuzi Tanzania



Qatar yaja na mkakati wa kuboresha huduma za afya



GAZA

Sitisho la vita labaki kwenye karatasi



Ajali Morogoro zilivyotikisa, Rais Samia aasa uangalifu

Ajali Morogoro zilivyotikisa, Rais Samia aasa uangalifu



Mamlaka zimeanza kutumia vipimo vya vinasaba (DNA) kutambua miili ya watu waliofariki katika ajali mbili zilizotokea mkoani Morogoro, huku Rais Samia Suluhu Hassan akitaka sheria za usalama barabarani zisimamiwe

k i k a -
mili-
f u

kuzuia majanga kama hayo.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka ndugu wa marehemu kufika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ili kutoa sampuli zitakazosaidia kutambua miili iliyoharibika vibaya kutokana na moto.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa Oktoba 9, jumla ya watu 32 walifariki na wengine 37 kujeruhiwa katika ajali mbili zilizotokea usiku wa Oktoba 8 kuamkia Oktoba 9.

Ajali ya kwanza ilitokea eneo la Mkambarani, ambapo basi lililokuwa likisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya liligongana uso kwa uso na lori lililobeba miti ya milunda. Baada ya kugongana, basi hilo lilishika moto na kutekelea, na kusababisha vifo vya watu 28.

Kutokana na kuungua kwa basi hilo, miili ya baadhi ya marehemu iliharibika kiasi cha kufanya utambuzi wa kawaida kuwa mgumu, hivyo mamlaka kuanza kutumia teknolojia ya DNA kusaidia kuthibitisha utambulisho wao.

Ajali ya pili ilitokea eneo la Miti Bora, kati ya Dakawa na Dumila, ikihusisha gari la Polisi na lori. Tukio hilo lilisababisha vifo vya watu wanne, wakiwamo askari polisi watatu.

Katika salamu zake za rambirambi, Rais Samia aliwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa wote waliofariki, huku akiwataki majeruhi kupona haraka.

Rais alilitaka Jeshi la Polisi kuendelea kusimamia sheria za usalama barabarani na kuhakikisha hatua zinazostahili zinachukuliwa dhidi ya wanaokiuka sheria hizo.

Pia, aliwahimiza madereva na watumiaji wengine wa barabara kuzingatia sheria, kuwa waangalifu na kuchukua tahadhari wakati wote wanapotumia barabara.

Alisisitiza umuhimu wa uwajibikaji wa kila mtumiaji wa barabara katika kupunguza ajali zinazoweza kuzuilika na kulinda maisha ya wananchi.

Matukio hayo yameibua tena umuhimu wa kuimarisha usalama barabarani, ikiwamo uzingatiaji wa sheria, umakini wa madereva na hatua za kuzuia ajali zinazoweza kusababisha vifo na majeraha kwa watu wengi.



Qatar yaja na mkakati wa kuboresha huduma za afya



Serikali ya Tanzania na Ufalme wa Qatar zimekubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta ya afya, hatua inayotarajiwa kuongeza upatikanaji wa huduma za matibabu, kuboresha ubora wake na kupanua wigo wa huduma maalumu kwa wananchi.

Ushirikiano huo unatarajiwa kujumuisha uanzishwaji wa hospitali nchini Tanzania, ambapo DOC Medical Center inatarajiwa kuchangia vifaa tiba, madaktari na wataalamu wa afya ili kuimarisha uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alibainisha hayo Oktoba 9, 2029, baada ya kutembelea kituo hicho kinachotoa huduma za afya kupitia idara nane za tiba maalumu.

Kituo hicho kinaongozwa na mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wake, Dkt. Emmanuel Tolessa, ambaye amekuwa akisimamia utoaji wa huduma za matibabu kupitia idara zake maalumu.

Dkt. Mwinyi alisema mpango huo ni sehemu ya juhudi za kuimarisha miundombinu ya afya nchini na kupanua wigo wa huduma zinazopatikana kwa wananchi, hususan katika maeneo yanayohitaji huduma za kibingwa na vifaa tiba

vya kisasa.

Alieleza kuwa utekelezaji wa mpango huo utahusisha ushirikiano na Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Ushirikiano huo unatarajiwa kuweka msingi wa kuunganisha nguvu za Serikali, taasisi za hifadhi ya jamii na wadau wa sekta ya afya ili kuboresha huduma za matibabu na kuongeza uwezo wa vituo vya afya kuhudumia wananchi.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa, mradi huo pia unalenga kuanzisha huduma za hospitali na famasia, hatua inayotarajiwa kupanua huduma zitakazopatikana kupitia mpango huo.

Uanzishwaji wa hospitali hiyo unaweza kuwa fursa ya kuongeza upatikanaji wa huduma za matibabu, huku mchango wa vifaa tiba na wataalamu ukitarajiwa kusaidia kuimarisha uwezo wa kutoa huduma za kitaalamu kwa wagonjwa.

Katika sekta ya afya, upatikanaji wa wataalamu wenye ujuzi, vifaa tiba na miundombinu inayokidhi mahitaji ya wagonjwa ni miongo-

ni mwa mambo muhimu katika kuboresha huduma. Hivyo, ushirikiano kati ya Tanzania na Qatar unatarajiwa kuwa sehemu ya juhudi za kuongeza uwezo wa sekta hiyo kukidhi mahitaji ya wananchi.

Aidha, ushiriki wa NSSF na PSSSF katika mpango huo unaonesha umuhimu wa kushirikisha taasisi za hifadhi ya jamii katika mipango inayolenga kuboresha huduma za afya.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika katikati ya mwaka 2027, huku utekelezaji wake ukitarajiwa kuweka msingi wa kuanzishwa kwa huduma za hospitali na famasia.

Hatua hiyo inakuja wakati ambapo upatikanaji wa huduma bora za afya unaendelea kuwa sehemu muhimu ya juhudi za kuboresha ustawi wa wananchi. Kupitia ushirikiano huo, Serikali na wadau wake wanatarajiwa kuongeza nguvu katika kuboresha miundombinu, upatikanaji wa vifaa tiba na huduma za kitaalamu.

Hata hivyo, mafanikio ya mpango huo yatategemea utekelezaji wake kwa wakati, upatikanaji wa wataalamu na vifaa tiba vinavyohitajika, pamoja na uwezo wa huduma zitakazoanzishwa kukidhi mahitaji ya wananchi.



Taaluma, dini na stadi za maisha zatajwa nguzo za malezi

Elimu ya darasani, malezi ya kiroho na stadi za maisha zimetajwa kuwa nguzo tatu muhimu za kuwaandaa vijana kukabiliana na changamoto za maisha na kuwawezesha kuchangia maendeleo ya jamii. Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa The Islamic Foundation, Arafat Badru, amesema hayo wakati akimwakilisha Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Aref Nahdi, katika mahafali ya Jumuiya ya TAMSIA Mkoa wa Morogoro.

Badru alisema elimu ya darasani pekee hai-toshi kumwandaa kijana kwa maisha, hivyo kuna umuhimu wa kuunganisha taaluma na malezi ya kiroho, maadili na uwezo wa kutu-

mia maarifa katika mazingira halisi ya maisha.

“Kuwaandaa vijana hakupaswi kuishia katika kuwapatia elimu ya darasani pekee, bali kunapaswa kuhusisha pia malezi ya kiroho, maadili na kuwajengea uwezo wa kutumia elimu wanayoipata kwa manufaa yao na jamii kwa ujumla,” alisema Badru.

Alieleza kuwa pamoja na kuwapatia vijana elimu itakayowawezesha kufaulu mitihani na kuendelea na masomo, wanapaswa pia kujengewa misingi imara ya dini na tabia njema itakayowaongoza katika kufanya maamuzi sahihi.

Aidha, alisema vijana wanahitaji kuandaliwa kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha kwa kuwajengea uwezo wa kujitambua, kutumia vipaji vyao na kuitumia elimu waliyoipata kujiletea maendeleo.

Katika kufanikisha hilo, Badru aliahidi kuwa The Islamic Foundation itaendelea kushirikiana na TAMSIA katika kuimarisha malezi na maandalizi ya wanafunzi wa Kiislamu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa The Islamic Foundation Mkoa wa Tanga, Sheikh Ally Ajiran, amewataka wanafunzi kudumisha misingi ya dini, kuwaheshimu wazazi na walimu pamoja na kuwa na nidhamu na bidii katika kutafuta elimu.

Alisema mahafali yanapaswa kuwa fursa ya kuwapatia vijana nasaha na kuwaandaa kwa hatua zinazofuata za maisha, ikiwamo kuendelea na elimu ya juu na kutimiza majukumu yao katika jamii.

Wanafunzi walioshiriki mahafali hayo wameishukuru The Islamic Foundation kwa mchango wake katika safari yao ya elimu, pamoja na wazazi na walimu waliowasaidia kufikia hatua hiyo.

Kongamano la kwanza la uwekezaji halal Tanzania

■ CIFCA, Taqseem Academy watia nguvu

Kampuni ya Shirkah Invest imeandaa kongamano la kwanza la uwekezaji halali nchini Tanzania, likilenga kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu fursa za uwekezaji unaozingatia misingi ya Sharia na kuhamasisha matumizi ya mitaji hiyo katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Kongamano hilo, lijulikanalo kama Tanzania Halal Investment Summit, litafanyika Novemba 12, 2026, katika Hoteli ya Hyatt Regency, Dar es Salaam, likiandaliwa kwa kushirikiana na Kituo cha Fedha za Kiislamu, Uzingatiaji na Ushauri (CIFCA) na Taqseem Academy.

Akizungumza na Gazeti IMAAN, Muandaaji wa tukio hilo na wa Shirkah, Salum Awadh, alisema kongamano hilo limeandaliwa wakati sekta ya uwekezaji nchini ikien-delea kukua, lakini Waislamu wengi wakiwa bado wanashiriki katika uwekezaji usiozingatia misingi ya Sharia.

“Sekta ya uwekezaji inakuwa kwa kasi na idadi ya wawekezaji inaongezeka, lakini bado Waislamu wengi wapo kwenye uwekezaji usio wa halal. Jukwaa kama hili litasaidia kutoa elimu na ufahamu wa kutosha juu ya aina mbalimbali za uwekezaji wa halal,” alisema.

Awadh alisema kongamano hilo, lenye kaulimbiu “Halal Investing Towards a US\$1 Trillion Economy”, litajadili mchango wa huduma za fedha za Kiislamu, hususan uwekezaji halali, katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Alisema waandaaji wamemwalika Waziri wa Fedha kuwa mgeni rasmi ili kutoa fursa ya kujadili namna Serikali inavyoweza kutumia huduma za fedha za Kiislamu kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo.

“Tunataka Waziri wa Fedha aondoke na mtazamo kwamba huduma za fedha za Kiislamu zina mchango mkubwa katika Dira 2050, hivyo Serikali iweke mazingira sahihi ya kutumia huduma hizi kwa ajili ya miradi mikubwa ya Serikali,” alisema.

Kwa mujibu wa Awadh, kongamano hilo pia

linalenga kuibua mjadala kuhusu changamoto ya upatikanaji wa mitaji inayozingatia Sharia kwa wafanyabiashara na wajasiriamali, suala ambalo alisema halijapewa nafasi ya kutosha katika majadiliano ya uwekezaji nchini.

Alisema katika hatua ya kuonyesha fursa zilizopo, waandaaji wametenga nafasi kwa kampuni changa tano kuwasilisha miradi yao mbele ya wawekezaji katika kipengele maalumu cha startup pitching.

Uwasilishaji huo utawapa wajasiriamali nafasi ya kutafuta mitaji na kujenga uhusiano na wawekezaji wanaotafuta biashara zinazokidhi masharti ya uwekezaji halali.

Kila kampuni itapewa dakika saba kuwasilisha mradi wake na dakika tano kujibu maswali ya wawekezaji, huku matokeo na nia ya wawekezaji kuwekeza vikitarajiwa kutangazwa siku hiyo.

Wataka sheria za fedha za Kiislamu

Awadh alisema kongamano hilo litatoa pia nafasi ya kujadili mazingira ya kisera na kisheria yanayohitajika ili kuimarisha huduma za fedha za Kiislamu nchini.

Alizitaja Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuwa miongoni mwa taasisi zilizoalikwa kushiriki.

“Tumealika pia taasisi simamizi kama vile BoT na CMSA ili kujadili masuala ya sera na sheria za huduma za fedha za Kiislamu, ili tutoke kuwa tu na kanuni na miongozo na sasa twende kwenye sheria kamili,” alisema.

Akizungumzia upekee wa

kongamano hilo, Awadh alisema tofauti na mikutano mingine inayojadili masuala mbalimbali ya fedha za Kiislamu, kongamano hili limejikita katika uwekezaji pekee na uhusiano wake na maendeleo ya uchumi wa taifa.

Alisema kipengele cha kampuni changa kuwasilisha miradi mbele ya wawekezaji ni sehemu nyingine inayolitofautisha na makongamano yaliyotangulia.

Kwa mujibu wa programu iliyotolewa na waandaaji, kongamano linatarajiwa kushirika wazungumzaji na wachangiaji 18, mihadhara mikuu mitatu na mjadala mitatu.

Mada zitakazojadiliwa ni pamoja na hali ya fedha za Kiislamu Afrika Mashariki, upatikanaji wa mitaji inayozingatia Sharia kwa biashara ndogo na za kati, viwango vya kuchunguza uhalali wa uwekezaji na fursa zilizopo katika sekta mbalimbali za uchumi.

Miongoni mwa wazungumzaji waliotangazwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Fahad Soud Hamid; mwana-benki na mhadhiri Dk. Muhsin Masoud, aliyewahi kuongoza Amana Bank na PBZ; pamoja na Awadh mwenyewe.

Kongamano hilo pia litajadili mwenendo wa fedha za Kiislamu duniani na uzoefu unaoweza kutumiwa na Tanzania kupanua huduma hizo.

Washiriki wanaolengwa ni wawekezaji binafsi, benki zinazotoa huduma za Kiislamu, taasisi za takafu, kampuni za uwekezaji, wajasiriamali, watunga sera, wataalamu wa Sharia na wanafunzi wa taaluma za fedha.



Wataalamu waenzi mchango wa waqf, wataka mageuzi Tanzania

WATAALAMU wa masuala ya waqf wametaka mageuzi ya kisheria na kiutawala katika usimamizi wa mali hizo nchini Tanzania, wakisema changamoto za umiliki, ukosefu wa uadilifu, utaalamu na uwazi zimepunguza mchango wake katika maendeleo ya jamii.

Wito huo umetolewa katika mjadala wa mtandaoni ulioandaliwa na Baitul Maal Tanzania, Oktoba 9, 2026, wenye mada ya “Ukosefu wa Uaminifu katika Utawala wa Waqf Tanzania: Tatizo Liko Wapi?”, ambapo mtoa mada mkuu alikuwa Sheikh Ponda Issa Ponda.

Sheikh Ponda alisema licha ya Tanzania kuwa na historia kubwa ya waqf katika kuenyeleza elimu, uchumi na huduma za kijamii, manufaa yake yamepungua kutokana na changamoto za kisheria na kiutawala.

“Tulipata manufaa nyuma lakini sasa hivi hatuna manufaa kwa ujumla ya waqf kama tunavyoona hivi sasa, au eidha manufaa yaliyopo ni madogo sana kulinganisha na spidi kubwa tuliyokuwa nayo huko nyuma,” alisema.

Alitaja uingiliaji wa mamlaka za serikali katika shughuli za taasisi za Kiislamu, hasa kuvunjwa kwa East African Muslim Welfare Society mwaka 1968 na kuhamishwa kwa mali zilizokuwa chini ya jumuiya hiyo, kuwa miongoni mwa sababu zilizodhoofisha maendeleo ya waqf nchini.

Alidai kuwa hatua hizo zilisababisha watoaji kupoteza imani katika usimamizi wa mali zao, hivyo kupunguza utoaji wa waqf na mapato yaliyokuwa yakitumika kugharamia huduma mbalimbali.

“Kwanza kabisa ni kwamba utoaji wa waqf ulisita. Maana yake watoaji walikata tamaa baada ya kuona kwamba kile ambacho wanakitoa sasa hakina usimamizi na wanaona kama wamepoteza,” alisema.

Katika kurekebisha hali hiyo, Sheikh Ponda alitaka kuanzishwa kwa Tume ya Waqf na Mahakama ya Kadhi, akisema vyombo hivyo vingesaidia kulinda mali, kuthibitisha masharti ya watoaji na kusuluhisha migogoro inayohusisha watoaji, wasimamizi na wanufaika.

Alisema pia kuna haja ya kuimarisha uadili-

fu na utaalamu wa viongozi wanaosimamia mali za waqf, pamoja na kuweka mfumo wa ukaguzi wa wazi na utoaji wa taarifa za mapato na matumizi kila mwezi.

“Tutague viongozi ambao ni waadilifu, uongozi ambao ni waeledi ambao wanaweza kusimamia yale mambo ipasavyo, lakini ni wabunifu ambao wanaweza kuendeleza zile waqf zikasimama vizuri,” alisema.

Sheikh Ponda pia alizungumzia changamoto za mali za waqf zilizokuwa chini ya taasisi mbalimbali, ikiwamo Msikiti wa Manyema, ambao alisema kihistoria ulikuwa na nyumba nyingi za biashara eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, lakini idadi yake imepungua.

Alidai kuwa baadhi ya mali za waqf nchini zimeuzwa au kushindwa kuwanufaisha walengwa kutokana na usimamizi usiofaa. Alihoji pia matumizi ya mapato ya baadhi ya vitega uchumi vilivyo chini ya BAKWATA.

Madai hayo kuhusu umiliki, mauzo na matumizi ya mali yanahitaji uthibitisho wa nyaraka na majibu ya taasisi zinazohusika.

Elimu na usimamizi wa kitaalamu

Akichangia mjadala, Salum Awadh alipendekeza Awqaf Tanzania, kwa kushirikiana na taasisi nyingine, kuandaa miongozo itakayowasaidia wananchi kuchagua wasimamizi wenye uwezo na uadilifu kabla ya kukabidhi mali zao.

Alisema taasisi hizo zinapaswa kufanyiwa uchunguzi wa uwezo, historia ya utendaji, mifumo ya uongozi na uzingatiaji wa masharti ya waqf.

Pendekezo hilo liliungwa mkono na Sheikh Ponda, ambaye alitaka litekelezwe haraka huku vigezo vya kuchagua taasisi vikiwa wazi.

Kwa upande wake, Sheikh Salum Lupande alisema usimamizi wa waqf unapaswa kuachana na mazoea na kuzingatia utaalamu wa kuendesha mali na uwekezaji, badala ya kutegemea elimu ya sheria za Kiislamu pekee.

Washiriki walisisitiza pia elimu kwa jamii kuhusu namna ya kutoa waqf, kuandaa mikataba na kuhakikisha masharti ya watoaji yanazingatiwa.

Mchango wa waqf waenziwa

Pamoja na changamoto hizo, wataalamu walieleza kuwa waqf ni miongoni mwa mifumo muhimu ya Kiislamu iliyochangia maendeleo ya elimu, afya, uchumi na ustawi wa jamii katika historia.

Sheikh Ponda alikumbusha kwamba utamaduni wa waqf ulianza tangu zama za Maswahaba, akitolea mfano Umar bin Al-Khattab aliyetoa ardhi yake ya Khaibar kuwa waqf kwa maelekezo ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Alimtaja pia Uthman bin Affan kuwa miongoni mwa Maswahaba walioacha mali za waqf zilizowasaidia watu kwa vizazi mbalimbali.

Katika kueleza mchango wa waqf duniani, Sheikh Ponda alitaja Chuo Kikuu cha Al-Azhar nchini Misri na Al-Qarawiyyin nchini Morocco kuwa mifano ya taasisi za elimu ambazo maendeleo yake yamehusishwa na mali za waqf.

Alisema Dola ya Ottoman pia ilitumia waqf kugharamia ujenzi na uendeshaji wa shule, hospitali, misikiti, huduma za maji na miundombinu mingine ya kijamii.

Akiongezea hoja hiyo, Salum Awadh alisema waqf ulikuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Dola ya Ottoman, akitaja makadirio kwamba wakati fulani mchango wake ulizidi asilimia 50 ya mapato ya serikali.

Alieleza kuwa mfumo huo uliwezesha kutoa huduma katika hatua zote za maisha ya mwanadamu, kuanzia kuzaliwa hadi kufariki dunia.

“From cradle to the grave,” alisema, akieleza namna watu walivyoweza kuzaliwa katika hospitali za waqf, kusoma kwenye shule zilizogharamiwa na waqf, kupata chakula na matibabu, hadi kugharamiwa sanda baada ya kufariki.

Hata hivyo, takwimu ya mchango wa zaidi ya asilimia 50 inahitaji uthibitisho wa kihistoria kuhusu kipindi na aina ya mapato yaliyohusika.

Kwa upande wa Tanzania, Sheikh Ponda alitaja taasisi za zamani, zikiwamo Tanga Muslim Association, Muslim Education Board, Arusha Muslim Union na Dodoma General Muslim Association, kuwa mifano ya jumuiya zilizotumia mali za waqf kuendeleza huduma za jamii.

Mwinyi atoa njia ya kukabiliana na changamoto za ajira Ghuba

■ Ushirikiano kati ya Afrika na nchi za Ghuba unatajwa kuwa muhimu katika kujenga mfumo wa ajira unaolinda haki za wafanyakazi wahamiaji, huku changamoto kubwa ikiwa ni kuhakikisha makubaliano ya kisiasa yanatekelezwa na kuleta mabadiliko katika maisha yao.

Wakati ajira katika nchi za nje zikien-delea kuwa fursa kwa watu wanaotafuta kipato na kuboresha maisha ya familia zao, suala la usalama, haki na uwajibikaji kwa wafanyakazi wahamiaji limeendelea kuhitaji ushirikiano wa karibu kati ya nchi wanazotoka na zile wanakoenda kufanya kazi.

Hilo ni miongoni mwa masuala yaliyopewa uzito katika Mkutano wa Pili wa Doha kuhusu Uhamaji Salama wa Wafanyakazi, uliofunguliwa Dar es Salaam, Oktoba 6, 2026, huku

Tanzania ikisisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa ya Afrika na nchi za Ghuba.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali

Mwinyi, aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa mkutano huo, amesema ni muhimu kuhakikisha uhamaji wa wafanyakazi unakuwa salama, wenye haki, unaozingatia taratibu na wenye manufaa kwa pande zote.

Ujumbe huo unaweka mkazo katika suala muhimu zaidi ya mikutano ya kimataifa: namna ya kuhakikisha maazimio yanayofikiwa yanabadilika kuwa mifumo inayotekelezeka na inayoweza kuwanufaisha wafanyakazi, familia zao, waajiri na uchumi wa nchi husika.

Kwa mujibu wa Dkt. Mwinyi, ahadi za kisiasa zinapaswa kugeuzwa kuwa sera, makubaliano na programu zinazotekelezeka ili kuboresha maisha ya wafanyakazi wahamiaji. Kauli hiyo inaweka wazi umuhimu wa nchi husika kuimarisha mifumo ya uajiri, kulinda haki za wafanyakazi na kuweka mikataba ya pande mbili inayobainisha wajibu wa kila upande.

Takwimu na sera za ajira

Dkt. Mwinyi pia amesisitiza umuhimu wa kutumia takwimu sahihi katika kupanga sera za uhamaji wa wafanyakazi.

Takwimu zinaweza kusaidia nchi kuelewa mwenendo wa uhamaji, mahitaji ya soko la ajira na changamoto zinazowakabili wafanyakazi katika nchi wanazokwenda kufanya kazi. Taarifa hizo pia zinaweza kuwa msingi wa kupanga sera zinazolingana na mazingira halisi ya ajira.

Kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika, ushirikiano huo unatoa nafasi ya kujadili namna ya kuimarisha mifumo ya uajiri na kuhakikisha wafanyakazi wanapata taarifa sahihi kabla ya kuondoka kwenda kutafuta ajira nje ya nchi.

Hata hivyo, ili malengo hayo yafikiwe, ni muhimu kuwepo kwa uratibu wa taasisi zinazohusika na kazi, ajira na mahusiano ya kimataifa, pamoja na mifumo ya kufuatilia utekelezaji wa makubaliano.

Wajibu wa Afrika na Ghuba

Mkutano huo umekutanisha wajumbe kutoka nchi zaidi ya 33, zikiwemo za Afrika, wanachama wa Baraza la Ushirikiano la Nchi za Ghuba (GCC+), Jordan na Lebanon, pamoja na wawakilishi wa taasisi mbalimbali za kimataifa.

Ushiriki wa mataifa hayo unaweka jukwaa la kujadili masuala yanayohusu uhamaji wa wafanyakazi na namna ya kuimarisha ushirikiano kati ya nchi zinazotuma na kupokea nguvu kazi.



MIMBARI ZETU

IMEANDALIWA

Na Barnabas Mkwaju

0766 364 354


KUTOKA

Masjid Nurah
(Msamvu, Morogoro)

Masjid Al-Haram
(Makka)

Masjid Haqq
(Karume, Morogoro)

Masjid Al Muizzu



MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA

IMAMU NA KHATIBU SHEIKH DKT. ABDULRAHMAN AL-SUDAIS



Sheikh Sudais aonya matumizi mabaya ya akili unde (AI)

MAKKA. Imamu na Khatibu wa Msikiti Mtukufu wa Makka, Sheikh Dkt. Abdulrahman Al-Sudais, amewaonya Waislamu dhidi ya kutumia teknolojia ya akili unde (AI) kughushi picha, video na sauti za watu, akisema vitendo hivyo ni uongo unaokatazwa na Uislamu.

Katika khutba ya Ijumaa, Oktoba 9, 2026, Sheikh Sudais alisema maendeleo ya teknolojia na mitandao ya kijamii ni neema kutoka kwa Allah, lakini matumizi yake yanapaswa kuzingatia misingi ya Sharia na maadili mema.

Alieleza kuwa kutumia akili unde kuiga sauti, kutengeneza video za kughushi, kujifanya mtu mwingine au kumnasibisha mtu kauli ambazo hakuzitoa ni udanganyifu unaoweza kuharibu heshima na haki za watu.

Aidha, alionya dhidi ya utapeli wa kifedha kupitia mitandao, ujumbe wa uongo unaoahidi utajiri wa haraka, udukuzi wa simu na kompyuta, vitisho vya kusambaza taarifa binafsi na kuvunja faragha za watu.

Akizungumzia wajibu wa kutumia mitandao kwa uangalifu, alisema mtu atawajibika mbele ya Allah si kwa maneno anayoyasema pekee, bali pia kwa taarifa anazoandika, kusambaza au kuchapisha upya.

Alirejea Qur'an inayosema hakuna neno analolitamka mwanadamu isipokuwa kuna malaika anayeliandika [Qur'an, 50:18].

Sheikh Sudais aliwataka Waislamu kuthibitisha usahihi wa habari kabla ya kuzisambaza, akirejea agizo la Qur'an la kuchunguza taarifa ili kuepuka kuwadhuru wengine kwa kutokujua [Qur'an, 49:6].

Pia alikumbusha hadithi ya Mtume Muhammad (SAW) inayosema kwamba inamtosha mtu kuwa muongo kwa kusimulia kila anachokisikia.

MSIKITI WA MTUME, MADINA

IMAM NA KHATIBU DK. KHALID AL-MAHNA



Sheikh Mahna ahimiza kauli njema, kutunza ulimi

IMAMU na Khatibu wa Msikiti wa Mtume mjini Madina, Sheikh Dk. Khalid Al-Mahna, amewataka Waislamu kujiepusha na lugha chafu, matusi na kauli zinazozua uadui, akisema maneno mazuri ni miongoni mwa mambo yanayomfikisha mja katika radhi za Allah.

Katika khutba ya Ijumaa, Oktoba 9, 2026, Sheikh Al-Mahna alisema tabia njema ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) ilikuwa mfano bora wa namna Muislamu anavyopaswa kuzungumza na watu.

Alieleza kuwa Mtume alikuwa mpole katika mazungumzo, aki-chagua maneno mazuri na kuepuka lugha kali, matusi na maneno ya kuwaudhi wengine.

Sheikh Al-Mahna alisema kauli njema zina nafasi kubwa katika kuimarisha uhusiano, kuunganisha nyoyo na kusuluhisha migogoro katika jamii.

Akirejea Qur'an, alikumbusha amri ya Allah inayowataka Waumini kusema maneno yaliyo bora zaidi kwa kuwa Shetani hutumia kauli mbaya kuzua mifarakano (Qur'an, 17:53).

Alisema mtu anapaswa kufikiri kabla ya kuzungumza, kwani neno moja linaweza kuwa sababu ya kupata radhi za Allah au ghadhabu Zake.

Aliwahimiza pia Waumini kuonyesha upole wanapowazungumzia maskini, wenye matatizo na wanaohitaji msaada, hata pale wana-poshindwa kuwasaidia.

Akihitimisha, alikumbusha kuwa neno zuri ni sadaka na linaweza kumpa faraja mwenye huzuni, kuondoa uadui na kuimarisha upendo katika jamii.

Alisisitiza kuwa Muislamu anapaswa kulinda ulimi wake dhidi ya kauli zinazodhalilisha wengine, kusambaza chuki au kuchochea migogoro. Badala yake, anapaswa kutumia maneno yenye hekima, heshima na manufaa kwa watu wanaomzunguka.

MASJID NURA, MSAMVU, MORO SHEIKH TAWAKAL HUSSEIN



Sheikh Tawakal awataka Waislamukuwa na yakini ya dua

Waumini wa Kiislamu wametakiwa kujenga moyo wa kuridhika na kile walichoruzukiwa na Allah (Subhanahu wa Ta'ala), huku wakien-delea kumuomba kwa yakini, subira na kutokuwa na wasiwasi kuhusu lini na kwa namna gani dua zao zitajibiwa.

Akitoa khutba ya Ijumaa katika Msikiti wa Nura, Msamvu, Morogoro, Sheikh Tawakkal Hussein alisema kuridhika na riziki ndogo ni miongoni mwa alama za uchamungu, zinazomsaidia Muislamu kuishi kwa utulivu wa moyo bila kutawaliwa na tamaa ya kutaka zaidi.

Katika khutba yake iliyokuwa na mada ya Ibada yenye athari kubwa sana katika maisha ya Muislamu, Sheikh Tawakkal alisisitiza umuhimu wa kuwa na yakini kwamba Allah amewaahidi waja Wake kuitikia wanapomuomba kwa kufuata maelekezo na adabu zinazotakiwa. Alisema waumini hawapaswi kuzama katika hofu, mashaka na wasiwasi kuhusu muda au namna ambayo maombi yao yatakavyojibiwa, kwa kuwa jambo la msingi ni kuendelea kumuomba Allah kwa imani na unyenyekevu.

“Maadamu Allah Subhanahu wa Ta'ala ameahidi kwamba kila atakayemuomba atamjibu, hakuna sababu ya kufikiria sana, kuogopa au kuwa na wasiwasi kuhusu namna na wakati wa kujibiwa,” alifundisha Sheikh Tawakkal.

Alieleza kuwa imani hiyo inapaswa kuambatana na kuzingatia masharti na adabu za dua, badala ya mtu kukata tamaa anapokosa kuona majibu anayoyatarajia kwa wakati anaoutaka.

Ujumbe huo unawakumbusha Waislamu kuwa maisha ya kiimani yanahitaji subira, kuridhika na kumtegemea Allah katika kila hali. Muislamu anapaswa kuendelea kufanya dua kwa yakini, huku aki-pokea riziki yake kwa shukrani na kuepuka kulinganisha maisha yake na ya wengine.

MASJID IMAAM BUKHARY, MORO SHEIKH JUMA DAHABU



Sheikh Dahabu: Msipoteze fursa ya ibada za usiku

Waislamu wametakiwa kuutumia wakati wa usiku kwa ibada, dua, istighfari na toba, badala ya kuupoteza katika mitandao ya kijamii na shughuli zisizo na manufaa kwa maisha yao ya dunia na Akhera.

Akitoa khutba ya Ijumaa katika Masjid Imaam Bukhary, Kihonda Maghorofani, Morogoro, Sheikh Juma Dhahabu alisema usiku ni miongoni mwa nyakati muhimu ambazo Muislamu anapaswa kuzitumia kujikurubisha kwa Allah Subhanahu wa Ta'ala na kujiandaa kwa maisha ya Akhera.

Katika khutba hiyo iliyokuwa na mada ya Wakati wa Usiku, Sheikh Dhahabu alisisitiza kuwa kupoteza muda huo ni kuikosa fursa muhimu ya kumuomba Allah, kutubia makosa na kuomba msamaha kwa madhambi anayoyajua na asiyoyajua.

Alieleza kuwa sehemu ya usiku wa mwisho ina nafasi kubwa katika ibada ya dua na istighfari, akiwahimiza waumini kuamka na kutumia muda huo kumuomba Mola wao kwa unyenyekevu.

Alisema badala ya mtu kutumia saa nyingi akizunguka kwenye mitandao ya kijamii hadi Alfajiri, ni vyema akatenga muda kwa ajili ya ibada na kuhakikisha halikosi Swala ya Alfajiri.

“Ukiupoteza wakati wa usiku umepata hasara,” alisisitiza Sheikh Dhahabu, akieleza kuwa matumizi mabaya ya muda huo yanaweza kumnyima Muislamu fursa ya kupata kheri nyingi.

Aidha, aliwakumbusha waumini umuhimu wa rakaa mbili za Sunnah kabla ya Swala ya Alfajiri, akirejea kauli ya Mtume Muhammad (Swalla Allahu alayhi wa sallam) kwamba rakaa hizo ni bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake.

Khutba hiyo ilitoa wito kwa Waislamu kuutumia usiku kwa hekima, wakitambua kuwa ni fursa ya kuimarisha imani, kutafuta msamaha na kujiandalia Akhera.

Likizo ya El Nino fursa wazazi kuwashupalia watoto madrasa



Likizo ndefu ya wanafunzi kuanzia Novemba hadi Desemba si wakati wa mapumziko pekee, bali ni fursa kwa wazazi wa Kiislamu kuwajenga watoto wao katika misingi ya dini. Kuhudhuria madrassa, kujifunza Qur'an na maadili ni uwekezaji muhimu unaoweza kuacha alama katika maisha yao ya baadaye.

Likizo ya El Nino fursa wazazi kuwashupalia watoto madrasa

Serikali imetangaza ratiba ya kufungwa kwa shule kuanzia mwanzoni mwa Novemba hadi Desemba.

Ni likizo ya mwaka iliyochanganyika na hofu ya tahadhari dhidi ya madhara yanayoweza kusababishwa na mvua za El Nino. Ndio maana mwaka huu watoto wanaweza kukaa nyumbani kwa karibu miezi miwili kabla ya kurudi tena shuleni mwaka 2027 In Shaa Allah.

Kwa wazazi wa Kiislamu, kipindi hiki kinaweza kuwa fursa muhimu na adhimu ya kuhakikisha watoto wao wanapata muda wa kujifunza dini hasa kwa kuhudhuria madrasa.

Kwa miezi mingi ya mwaka, watoto hutumia sehemu kubwa ya muda wao shuleni. Asubuhi wanaondoka majumbani mapema, na wanaporudi, mara nyingi huwa wamechoka kutokana na masomo na shughuli nyingine za shule.

Hali hii imekuwa changamoto kwa baadhi ya wazazi wanaotamani watoto wao wapate elimu ya dini, lakini wanashindwa kuwaunganisha na ratiba ya madrasa ambapo sasa ratiba zake zimejikuta zikiishia hadi usiku.

Hata hivyo, likizo inapokuwa ndefu, changamoto hiyo inapungua. Mtoto anakuwa na muda wa kutosha wa kuhudhuria madrasa, kujifunza Qur'an, kusoma Hadith, kufahamu misingi ya ibada na kuelewa maadili yanayopaswa kuongoza maisha yake ya kila siku.

Hivyo, wazazi wanapaswa kuiona likizo hii kama nafasi ya kujenga msingi wa dini kwa watoto wao, badala ya kuiacha ipite kwa michezo, simu, televisheni na shughuli zisizo na manufaa ya kudumu.

Ni muhimu mzazi kutambua kuwa elimu ya mtoto haikamiliki kwa masomo ya darasani pekee. Mtoto

anahitaji pia kuelekezwa kuhusu namna ya kumuabudu Mwenyezi Mungu, kuheshimu wazazi, kuwatendea wema majirani, kuwa mwaminifu, kujiepusha na maovu na kuwajibika katika jamii.

Katika kipindi ambacho mtoto hana majukumu mengi ya shule, wazazi wanaweza kupanga ratiba maalumu inayomuwezesha kuhudhuria madrasa kila siku au kwa siku zinazopangwa na walimu wa dini. Wanaweza pia kufuatilia mahudhurio na kuhakikisha anachojifunza darasani kinaimarishwa nyumbani.

Kwa kufanya hivyo, mzazi hatakuwa amempeleka mtoto madrasa kwa ajili ya kujaza muda wa likizo, bali atakuwa amewekeza katika malezi yake ya muda mrefu.

Wakati ndio huu

Jamii ya Kiislamu inapokabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaadili, suala la malezi ya watoto haliwezi kupuuzwa. Watoto wanakua katika mazingira yenye taarifa nyingi, mitandao ya kijamii na ushawishi ambao wakati mwingine unaweza kuwapeleka katika tabia zisizolingana na misingi ya dini.

Miongoni mwa sababu zinazoweza kuchangia changamoto hizo ni ukosefu wa elimu na malezi ya kutosha ya dini tangu utotoni. Mtoto ambaye hajafundishwa misingi ya dini, maadili na wajibu wake anaweza kukosa msingi wa kumsaidia kutofautisha mema na mabaya.

Hapa ndipo jukumu la wazazi linapokuwa kubwa zaidi. Likizo hii ndefu iwe kipindi cha wazazi "kuwapika" watoto wao kwa malezi yenye

msingi ya dini. Si lazima kila jukumu liachwe kwa mwalimu wa madrasa.

Mzazi naye ana nafasi kubwa ya kumfundisha mtoto ndani ya nyumba kupitia vitendo, mazungumzo na mfano wa maisha. Mtoto aki-ona mzazi wake anazingatia swala, anaheshimu watu, anasema kweli na anajiepusha na tabia mbaya, anajifunza hata kabla hajaambiwa kwa maneno. Hivyo, elimu ya madrasa inapounganishwa na mfano wa wazazi nyumbani, mtoto hupata malezi yenye nguvu zaidi.

Wazazi pia wanaweza kutumia muda huu kuwafundisha watoto sura za Qur'an, dua, adabu za kula na kunywa, heshima kwa wazazi na wakubwa, pamoja na umuhimu wa kusaidia wengine.

Watoto wakubwa wanaweza kupewa majukumu ya kuwasaidia wadogo zao katika kusoma Qur'an na mambo mengine ya msingi ya dini.

Muhimu zaidi ni wazazi kutokubali likizo ipite bila mpango. Muda wa ziada unaopatikana unapaswa kutumiwa kwa manufaa ya mtoto.

Ikiwa miezi mingine ya mwaka mtoto amekuwa akishindwa kuhudhuria madrasa kwa sababu ya ratiba ya shule, basi likizo hii ni nafasi ya kurekebisha hali hiyo.

Kwa wazazi wa Kiislamu, huu si wakati wa kuuliza mtoto atafanya nini kwa siku nzima, bali ni wakati wa kupanga atajifunza nini, atasoma nini na atajengeka katika misingi gani.

Ikiwa watoto wataingia katika likizo wakiwa na ratiba nzuri ya madrasa na kutoka wakiwa wameongeza uelewa wao wa Qur'an, ibada na maadili, basi likizo hiyo itakuwa imeacha faida kubwa kuliko mapumziko pekee.

Hatua hiyo inanzia nyumbani. Wazazi wanapaswa kusimamia, kufuatilia na kuwahimiza watoto wao. Likizo hii ndefu isiwe kipindi cha kupoteza muda; iwe shule nyingine ya malezi, maadili na dini.

Ni fursa ambayo wazazi hawapaswi kuipuuza.



Moto wateketeza mabanda 17 ya wafanyabiashara Tanga



■ **Wafanyabiashara 17 jijini Tanga wanakabiliwa na wakati mgumu baada ya moto kuteketeza mabanda yao na kuangamiza mali walizotegemea kuendesha biashara, huku wakiomba msaada wa kurejesha mitaji na kuanza upya.**

Kwa wafanyabiashara walioathirika, changamoto iliyopo sasa si kupoteza mabanda pekee, bali pia namna ya kurejesha mitaji iliyoteketea na kuendelea na shughuli zilizokuwa chanzo cha kipato chao.

Moto huo uliozuka usiku wa kuamkia jana katika mtaa wa Miembeni B, kata ya Magaoni jijini Tanga, uliteketeza mabanda 17, na kuwacha wamiliki wake wakikabiliana na hasara ambayo tathmini yake bado haijakamilika.

Baadhi ya waathirika wamesema mali zote zilizokuwamo ndani ya mabanda hayo zime-teketea, huku mabaki yaliyosalia yakiwa haya-fai tena kwa biashara wala matumizi mengine.

Hali hiyo imeongeza ugumu wa kuanza upya kwa wafanyabiashara hao, ambao sasa wanaomba Serikali iwasaidie kurejesha mitaji yao iliyopotea.

Changamoto ya kuanza upya

Kwa biashara ndogo zinazotegemea mtaji wa

kila siku, kupotea kwa bidhaa na vifaa kunaweza kuathiri uwezo wa mmiliki kuendelea na shughuli zake. Moto unapoteketeza mali zote kwa wakati mmoja, mfanyabiashara hulazimika kutafuta fedha nyingine za kununua bidhaa na kurejesha eneo la biashara.

Hata hivyo, kiwango cha hasara kilichosababishwa na tukio hilo bado hakijafahamika rasmi, hivyo ukubwa wa mahitaji ya waathirika haujawekwa bayana.

Moto huo ulisambaa kutoka banda moja hadi jingine kutokana na uwepo wa mbao na vifaa vingine vya biashara, hali iliyofanya iwe vigumu kuokoa mali zilizokuwamo ndani ya mabanda hayo.

Serikali yafuatilia tukio

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Gilbert Kalima, alipotembelea eneo la tukio, alisema tathmini ya hasara bado haijakamilika na chanzo cha moto hakijafahamika.

Alisema uchunguzi unaendelea kubaini kilichosababisha moto huo, huku akiwataka wafanyabiashara walioathirika kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kigumu.

Kalima amesema Serikali itaendelea kushirikiana na waathirika wanapokabiliana na athari za tukio hilo.

Hatua za baadaye

Kwa sasa, wafanyabiashara hao wanakabiliwa na jukumu la kutafuta namna ya kurejesha shughuli zao, wakati uchunguzi na tathmini ya hasara vikiendelea.

Msaada wanaouomba unaweza kuwa muhimu katika juhudi za kuanza upya, ingawa aina na kiwango cha msaada utakaotolewa bado hakijabainishwa.

Tukio hilo pia linaweka mbele umuhimu wa kuimarisha hatua za kuzuia na kudhibiti moto katika maeneo ya biashara, ili kupunguza uwezekano wa majanga kama hayo.

Vitambulisho vya wazawa vyatumika katika biashara za wageni: Londo

■ Serikali imeibua wasiwasi kuhusu baadhi ya Watanzania wanaodaiwa kutumia majina na vitambulisho vyao kusajili makampuni kwa niaba ya wageni, ikionya kuwa hali hiyo inaweza kudhoofisha jitihada za kulinda nafasi za wazawa katika biashara na ajira.

Wakati Tanzania ikiendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, Serikali imeelekeza nguvu katika kufuatilia umiliki wa makampuni yanayosajiliwa kwa majina ya Watanzania, baada ya kubainika kwa kile ilichokitaja kuwa matumizi ya majina na vitambulisho vya wazawa kwa niaba ya wageni.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Dennis Londo, amesema vitendo hivyo vinahitaji ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha usajili wa biashara hauwi njia ya kukwepa taratibu zinazolenga kulinda ushiriki wa Watanzania katika shughuli za kiuchumi.

Londo alitoa kauli hiyo Oktoba 11, 2026, mkoani Morogoro, wakati akifunga kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), akiiagiza taasisi hiyo kutumia mifumo, utaalamu na uwezo wake kufuatilia suala hilo.

Alisemabaadhiya wageni wananguvukubwa za mitaji, ujuzi na teknolojia, hivyo kuna haja ya kuweka mikakati itakayowezesha Watanzania kushiriki katika biashara wanazoweza kuzifanya.

Umiliki wa biashara wahitaji ufuatiliaji

Hoja iliyotolewa na Serikali inaweka mbele

umuhimu wa kutofautisha kati ya umiliki halisi wa kampuni na jina linalotumika katika nyaraka za usajili.

Iwapo majina ya Watanzania yanatumika kuficha wamiliki halisi wa makampuni, mamlaka husika zinahitaji kuwa na uwezo wa kubaini wahusika, kufuatilia uhalali wa usajili na kuhakikisha taratibu za biashara zinafuatwa.

Hata hivyo, madai hayo yanahitaji kufanywa uchunguzi na kuthibitishwa kwa ushahidi wa mamlaka husika kabla ya kufikia hitimisho kuhusu kampuni au watu wanaohusika.

Kwa BRELA, changamoto hiyo inaongeza umuhimu wa kuimarisha mifumo ya usajili na uhakiki wa taarifa za kampuni, pamoja na ushirikiano na taasisi nyingine za Serikali katika kufuatilia umiliki na shughuli za biashara.

Hatua hizo zinaweza kusaidia kuboresha uwazi wa taarifa za kampuni na kuweka mazingira ambayo wafanyabiashara wanafuata sheria wanashindana kwa misingi inayotambuliwa.

Leseni za biashara zahitaji uratibu

Londo pia ameitaka BRELA kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha biashara ndogo na za kati zinarasimishwa.



Ameeleza kuwa leseni za biashara za kundi B hutolewa na halmashauri za wilaya, manispaa na majiji, badala ya BRELA, hivyo ushirikiano wa mamlaka hizo ni muhimu katika kuboresha usimamizi wa biashara.

Urasimishaji unaweza kusaidia kuboresha upatikanaji wa taarifa za biashara, kuimarisha ufuatiliaji wa shughuli za kiuchumi na kuweka msingi wa mazingira bora ya ushindani.

Aidha, katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Londo amesema BRELA ina nafasi muhimu katika kuongeza thamani ya bidhaa, kukuza uchumi wa viwanda na kulinda ajira za Watanzania.

Brela kuimarisha huduma

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, amesema taasisi hiyo itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kupitia mifumo ya kielektroniki, kushirikiana na mamlaka husika katika utoaji wa leseni za kundi B na kupitia sheria na kanuni ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Katika kikao hicho, Londo pia alizindua BRELA SACCOS Limited, chama cha akiba na mikopo kinacholenga kuimarisha ustawi wa watumishi kupitia utamaduni wa kuweka akiba na kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha.

Wafanyabiashara wapewa somo misingi 6 ya biashara ya halal

Katika biashara, faida pekee haitoshi; Muislamu anapaswa kutafuta riziki kwa njia inayompendeza Allah, akiepuka haramu na kusimamia haki, uadilifu na uaminifu katika kila muamala.

WAFANYABIASHARA Waislamu wametakiwa kuzingatia misingi sita ya Kiislamu katika shughuli zao, ikiwamo uaminifu, mtaji halali na elimu ya miamala, ili biashara zao zisiwe za kutafuta faida pekee, bali ziwe pia sehemu ya ibada inayowapatia malipo kutoka kwa Allah.

Wito huo umetolewa na Sheikh Khalfan Abdallah Mgeituff wakati akitoa mhadhara wenye mada ya “Biashara Ibadah na Misingi Yake” katika Msikiti wa Taqwa, Bungoni, wilayani Ilala, Dar es Salaam, hivi karibuni.

Sheikh Abdallah alisema biashara inaweza kuwa ibada ikiwa itafanywa kwa nia safi (ikhlas), elimu ya Sharia, mtaji halali, tabia njema, utoaji wa zaka na sadaka, pamoja na kushirikiana katika mambo ya kheri.

Alieleza kuwa Uislamu unaruhusu biashara na kutafuta faida, lakini unamtaka mfanyabiashara kuzingatia mipaka ya Sharia na maslahi ya wengine badala ya kutumia njia yoyote kujiipatia mali, huku akirejea Qur’an, alisema Allah amehalalisha biashara na kuharamisha riba [Qur’an, 2:275].

Msingi wa kwanza ni ikhlasi, yaani kufanya biashara kwa nia ya kutafuta radhi za Allah, kujipatia riziki halali, kuhudumia familia, kuwasaidia wazazi na wenye mahitaji, badala ya kutafuta utajiri kwa majivuno au kujionyesha, akikumbusha Hadith ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) inayosema kwamba matendo yanategemea nia.

Msingi wa pili ni elimu ya fiqhi ya miamala, inayomwezesha mfanyabiashara kutambua masharti ya mikataba ya mauzo, ukodishaji, ushirika na uwakala, pamoja na mambo yaliyoharamishwa katika biashara.

“Ukiulizwa sharti za mkataba wa kukodisha, sharti za kusihhi musharaka, riba na mambo mbalimbali yaliyokatazwa katika miamala tuta-

kimbiana hapa. Elimu ni msingi muhimu katika biashara ibada,” alisema.

Mengine ambayo wafanyabiashara wanapaswa kuyafahamu alitaja kuwa ni pamoja na riba, gharar (kutokuwa na uhakika mkubwa unao-katazwa katika mkataba), ihtikar (kuhodhi bidhaa ili kupandisha bei) na najash (kupandisha bei kwa udanganyifu bila nia ya kununua).

Msingi wa tatu ni mtaji halali, akisema biashara inayolenga kuwa ibada lazima ianzishwe na kuendeshwa kwa mali zinazotokana na vyanzo vinavyoruhusiwa na Sharia. Alitaja biashara ya pombe, bangi, mikopo yenye riba na mali zilizopatikana kwa wizi au dhulma kuwa miongoni mwa vyanzo vinavyopaswa kuepukwa.

Msingi wa nne ni akhlaqi, au tabia njema, ambapo Sheikh Abdallah alisema mfanyabiashara anapaswa kuwa mkweli, mwaminifu, mwadilifu, mwenye subira na anayewatendea wateja na wafanyakazi wake kwa wema.

Alikemea tabia ya kuficha kasoro za bidhaa, kuuza bidhaa bandia kama halisi, kupima pungufu na kutumia viapo vya uongo ili kushawishi wateja. “Yeye ataingia mjini, wewe utaingia motoni,” alisema, akionya dhidi ya wafanyabiashara wanaojivunia kuwahadaa wateja.

Alisisitiza umuhimu wa kumweleza mteja ukweli kuhusu bidhaa, hata kama kufanya hivyo kutapunguza uwezekano wa kuuzwa. “Mteja kaja, kachagua chenye kasoro, mjulishe kuwa kina kasoro, mfanyie wema,” alisema.

Kuhusu viapo, Sheikh Abdallah aliwakemea wafanyabiashara wanaotumia jina la Allah kuthibitisha madai yasiyo ya kweli. “Mtume kakataza kuapa hata kwa jambo la kweli... sasa wewe unayeapa kwa uongo hali yako ikoje? Yaani unatumia jina la Allah ili jambo lionekane la kweli,” alisema.

Alihimiza Waislamu wasimamishe biashara zao katika misingi ya taqwa, birri (wema),

swidqi (ukweli), uaminifu, uadilifu katika kulipa haki za wafanyakazi, kuwahurumia wadaiwa wanaopitia matatizo na kuwasaidia wateja pale inapowezekana.

Aliwakumbusha pia wafanyabiashara kutoruhusu shughuli za kutafuta riziki ziwasa-haulishe swala na kumdhukuru Allah, akirejea sifa ya Waumini ambao biashara haiwashughulishi kiasi cha kuacha ibada [Qur’an, 24:37].

Msingi wa tano ni zaka, sadaka na kumtegemea Allah, ambapo Sheikh Abdallah alisema mfanyabiashara ambaye mali yake imetimiza masharti ya zaka ana wajibu wa kuitoa, huku sadaka ikihimizwa kwa kila mwenye uwezo. Alieleza kuwa hata wafanyabiashara ambao hawajafikia kiwango cha kuwajibika kutoa zaka wanaweza kutoa sadaka kulingana na uwezo wao. Msingi wa sita ni ta’awuni, yaani kushirikiana na kusaidiana katika mambo ya kheri badala ya kujenga biashara katika ubinafsi, chuki na ushindani wa kukomoana.

Sheikh Abdallah alisema wafanyabiashara wanapaswa kushindana kwa njia halali, huku wakiepuka vitendo vya kuhujumu biashara za wenzao, kudanganya kwa pamoja au kupanga mbinu za kuumiza wateja. Akirejea Qur’an, alisema Allah amewaamrisha Waumini kushirikiana katika wema na uchamungu, wala si katika dhambi na uadui [Qur’an, 5:2].

Alitaja mfumo wa bima ya Kiislamu (takaful) kuwa mfano wa ushirikiano wa kiuchumi, ambapo washiriki huchangia mfuko wa pamoja kwa ajili ya kusaidiana pale mmoja wao anapopatwa na janga au hasara.

Akihitimisha mhadhara, Sheikh Abdallah aliwakumbusha Waislamu kwamba kutafuta riziki hakuhalalishi kutumia njia zilizokatazwa na Sharia.

Alinukuu Hadithi iliyopokewa na Jabir bin Abdallah inayohimiza kumcha Allah na kutafuta riziki kwa njia nzuri na halali, kwa kuwa hakuna nafsi itakayofariki kabla haijakamilishiwa riziki yake.

“Pupa za nini za kuingia kwenye haramu? Kama kila mtu kaandikiwa fungu lake, na kama tunaingiza Hadithi hii katika bongo zetu kisawa-sawa, kwa nini utumie njia za mkato za haramu, kwa nini utumie usanii?” alihoji.

Waqf ya fedha Tanzania yaanza kuimarika

MFUMO wa waqf ya fedha (Cash Waqf) umeanza kupata nafasi nchini Tanzania, ukitoa fursa kwa Waislamu kushiriki katika sadaka yenye manufaa ya kudumu bila kulazimika kumiliki mashamba, nyumba au mali nyingine kubwa.

Mfumo huo, unaojulikana katika fiqhi ya Kiislamu kama Waqf al-Nuqud, unamwezesha mtu kutoa kiasi cha fedha kinachowekezwa katika shughuli halali, huku mapato yanayopatikana yakitumika kugharamia huduma za kijamii kulingana na madhumuni ya mtoaji.

Akizungumza katika mjadala wa mtandaoni ulioandaliwa na Baitul Maal Tanzania, Oktoba 9, 2026, mtaalamu wa fedha za Kiislamu, Salum Awadh, alisema mfumo huo unaweza kuongeza ushiriki wa wananchi katika waqf na kupanua mchango wake katika maendeleo.

Alisema kihistoria, utoaji wa waqf ulihusishwa zaidi na mali zisizohamishika, hususan ardhi na majengo, hali iliyowafanya baadhi ya Waislamu kudhani kwamba hawawezi kushiriki bila kuwa na mali hizo.

“Sasa watu wengi walikuwa wanaona kama vile sasa mimi kama sina mali, mimi nitashiriki vipi kutoa waqf?” alisema.

Alieleza kuwa waqf ya fedha inatoa suluhisho kwa changamoto hiyo kwa kuruhusu michango ya fedha kukusanywa na kuwekeza, huku mtaji ukihifadhiwa ili kuendelea kuzalisha manufaa kwa walengwa.

Jitihada za hay-atul ulamaa na vid

Akieleza hatua zilizofikiwa nchini, Awadh alisema taasisi ya Umoja wa Wanazuoni Tanzania (Hay-atul Ulamaa) imeanzisha mfuko wa waqf ya fedha ambao hadi wakati wa mjadala ulikuwa umekusanya Sh milioni 40.

Alisema fedha hizo zimewekezwa katika sukuk, yaani hatifungani zinazozingatia misingi ya Sharia, na mfuko tayari umepokea malipo ya awali kutokana na uwekezaji huo.

“Mpaka sasa tushakusanya milioni 40 na zishawekezwa kwenye sukuk, na walishapata malipo ya mwanzo,” alisema.

Kwa mujibu wake, lengo likiwa kuhifadhi mtaji na kutumia mapato yake kusaidia shughuli za Hay-atul Ulamaa ikiwemo ujenzi wa vituo vya taasisi katika kanda mbalimbali, kuendeleza shughuli za da'wa na kusaidia masheikh wanaokabiliwa na matatizo ya kiafya.

Alisema utaratibu wa mfuko unagawa mapato ya uwekezaji kwa kuelekeza asilimia 80 kwa wanufaika, asilimia 15 katika kuongeza mtaji na asilimia tano kugharamia usimamizi.

Awadh alisema pia wameanza kushiriki ana na taasisi ya Volunteers in Development (VIP), ambayo imeweka lengo la kukusanya Sh bilioni moja kupitia waqf ya fedha, ingawa lengo hilo bado halijafikiwa.

Alitaja uelewa mdogo wa jamii kuhusu mfumo huo kuwa miongoni mwa changamoto zinazohitaji kushughulikiwa.

Elimu yahitajika

Awadh alisema kuongeza elimu kuhusu waqf ni muhimu ili wananchi waelewe namna ya kuchangia, jinsi fedha zinavyowekezwa na utaratibu wa kusimamia manufaa yake.

Alisisitiza pia umuhimu wa kuwa na nyaraka za waqf (waqfiyya) zinazobainisha madhumuni ya mtoaji, wasimamizi na walengwa, ili kuhakikisha fedha zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Sheikh Ponda Issa Ponda, aliyekuwa mtoa mada mkuu, alisisitiza umuhimu wa kuhuisha utamaduni wa kutoa waqf na kuimarisha mifumo ya usimamizi wake.

Alisema mali za waqf zina uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya Waislamu endapo zitasimamiwa kwa uadilifu na utaalumu.

Kwa mfumo wa waqf ya fedha, hata michango midogo ya wananchi inaweza kukusanywa na kuwa mtaji wa uwekezaji unaozalisha mapato kwa manufaa ya jamii kwa muda mrefu.

Uzoefu wa nchi nyingine

Awadh alisema mfumo wa waqf ya fedha umeendelea kutumika katika nchi mbalimbali, zikiwamo Malaysia, Indonesia na Afrika Kusini, ambako umesaidia kupanua wigo wa wananchi wanaoshiriki katika kutoa waqf.

Alitolea mfano taasisi ya Awqaf South Africa, ambayo amesema imeanzisha utaratibu unaowawezesha wafanyakazi kuchangia waqf moja kwa moja kutoka kwenye mishahara yao kila mwezi.

Kwa mujibu wake, wachangiaji huchagua maeneo wanayotaka kusaidia, yakiwamo elimu na huduma za kifedha kwa wajasiriamali kupitia mikopo isiyo na riba ya Qard Hasan.

Akizungumzia historia ya waqf kwa upana, Awadh alisema mfumo huo ulitoa mchango mkubwa katika ustawi wa jamii, akitoa mfano wa Dola ya Ottoman, ambapo huduma mbalimbali ziligharamiwa kupitia mali za waqf.

Alieleza kwamba waqf uliweza kumhudumia mtu katika hatua zote za maisha, kuanzia kuzaliwa hadi kufariki dunia, kupitia hospitali, shule, huduma za chakula na mahitaji mengine.



Hukumu ya u-CAG wa Prof. Assad yaacha somo

HUKUMU ya Mahakama ya Rufani ya Oktoba 6, 2026, iliyohibitisha kuwa kuondolewa madarakani kwa aliyekuwa Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, mwaka 2019 kulikuwa kinyume cha Katiba, imeacha mafunzo muhimu kuhusu utawala wa sheria, mipaka ya mamlaka na utetezi wa Katiba.

Wahenga walisema ukweli unaweza kuchelewa, lakini haupotei. Miakasaba baada ya Prof. Assad kuondolewa madarakani, Mahakama ya Rufani imeweka hitimisho la kisheria kuhusu hatua hiyo, ikiunga mkono uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu Desemba 5, 2022.

Prof. Assad aliteuliwa mwaka 2014 na kuondolewa Novemba 2019 kwa hoja kuwa kipindi chake cha miaka mitano kiliisha. Nafasi yake ilichukuliwa na Charles Kichere.

Safari hii ndefu ya kimahakama inatukumbusha thamani ya subira. Ingawa Prof. Assad hakurejeshwa madarakani wala kupewa fidia, kumbukumbu za kisheria sasa zimewekwa sawa kuhusu uhalali wa kuondolewa kwake.

Hukumu imekumbusha pia ukuu wa Katiba katika mfumo wa sheria. Mahakama ilithibitisha kuwa kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma cha mwaka 2008, kilichoweka ukomo wa miaka mitano unaoweza kuongezwa, kilikinza na Ibara ya 144(1) ya Katiba.

Kwa mujibu wa mahakama, Bunge lina

mamlaka ya kuweka umri wa kustaafu kwa CAG, lakini si mfumo tofauti wa vipindi vya kuhudumu unaoweza kumwondoa kabla ya umri huo. Katiba pia imeweka sababu na utaratibu maalumu wa kumwondoa CAG kabla ya kustaafu.

Hapa kuna fundisho kwa wenye mamlaka: kuwepo kwa sheria hakutoshi kuhafalisha hatua inayopingana na Katiba.

Katika sakata hili, mchango wa mwana-siasa Zitto Kabwe hauwezi kupuuzwa. Kupitia shauri alilofungua baada ya kuondolewa kwa Prof. Assad, ameyonesha umuhimu wa wananchi kutumia mahakama kutetea Katiba na uhuru wa taasisi zinazowajibika kusimamia fedha za umma.

Z i t t o

ameipongeza hukumu, lakini ametoridhishwa na kutotolewa kwa nafuu ya moja kwa moja kwa Prof. Assad.

Mahakama iliona kuwa kumrejesha Assad kungeathiri uteuzi halali wa aliyemrithi, huku ikikataa pia kutoa fidia katika shauri hilo la kikatiba.

Zaidi ya kusahihisha kumbukumbu za tukio la mwaka 2019, hukumu imeweka mwongozo wa kisheria kwa maamuzi yajayo kuhusu muda wa kuhudumu kwa CAG na mipaka ya mamlaka ya kumwondoa.

Hata hivyo, swali linabaki: Ikiwa ukiukwaji wa Katiba umethibitishwa, madhara aliyopata mhusika yashughulikiwe vipi?

Kwa jumla, hukumu hii inatukumbusha kwamba madaraka yana mipaka, Katiba inapaswa kuheshimiwa na wananchi wana nafasi ya kuulinda. Zaidi ya yote, ukweli unaweza kuchukua muda mrefu kuthibitishwa, lakini thamani yake katika kuweka historia sawa haipotei.



Tetemeko Kagera laamsha kumbukumbu za maafa ya 2016

TETEMEKO la ardhi lililotokea mkoani Kagera Oktoba 9, 2026, limeamsha kumbukumbu za maafa ya mwaka 2016 yaliyosababisha vifo vya watu 17, mamia kujeruhiwa na maelfu kupoteza makazi yao.

Tetemeko hilo, lililokadiriwa kuwa na ukubwa wa kati ya 5.0 na 5.2, lilitokea saa 11:24 alfajiri na kuzua hofu miongoni mwa wakazi baada ya nyumba zao kutikisika.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Kanali Yahaya Kido, alisema hali ya usalama ilikuwa shwari baada ya tukio hilo, huku Kitengo cha Maafa kikiendelea kufuatilia iwapo kulikuwa na

madhara.

Aliwataka wananchi kuwa watulivu, kufuata maelekezo ya wataalamu na kutoa taarifa kwa mamlaka wanapobaini athari za tetemeko.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima, alisema nyumba yake pia ilitikisika kwa nguvu, huku akipokea simu kutoka kwa wananchi waliokuwa wameingia na hofu. "Hata nyumba yangu, iliyofanywa ukarabati takribani miaka miwili iliyo-pita, ilitikisika kwa nguvu," alisema.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari,

hususan wanaoishi katika majengo yenye nyufa, yaliyochakaa au ambayo ujenzi wake haujakamilika.

Tetemeko hilo limewakumbusha wakazi maafa ya Septemba 10, 2016, wakati tetemeko la ukubwa wa 5.9 lilipoikumba Kagera na kuharibu maelfu ya nyumba.

Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), watu 17 walifariki na 440 kujeruhiwa katika maafa hayo, huku nyumba zaidi ya 2,000 zikiharibiwa kabisa na nyingine zaidi ya 14,000 kupata uharibifu wa sehemu.



Hili la elimu ya zaka lipewe kipaumbele

Miongoni mwa mambo ambayo tumekuwa tuki- yasisitiza mara kwa mara katika gazeti hili ni umuhimu wa kutekeleza nguzo ya zaka. Hata leo tunalazimika kuisitiza umuhimu wake, kwa kuamini kwamba zaka inapaswa kuwa miongoni mwa vipaumbele vya Waislamu.

Ulazima wa kuisitiza nguzo hii unatokana na kauli ya mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM), Dkt. Bilal Majuva aliyoitoe hivi karibuni kwamba zaka inaweza kuchangia katika kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Kwa mujibu wa Dkt. Majuva, zaka inaweza kuwa nyenzo muhimu katika kupunguza umasikini na njaa, kuboresha huduma za afya na elimu, kuongeza fursa za ajira na kipato, kuwezesha upatikanaji wa maji safi, na kupunguza pengo la kipato.

Dkt. Majuva alikuwa akiwasilisha mada katika semina iliyofanyika katika Msikiti wa Nunge jijini Dodo-

ma, iliyoandaliwa kwa ushirikiano wa Baitulmaal Tanzania na TAM-PRO SACCOS Dodoma kwa lengo la kueneza elimu ya zaka mikoani.

Miongoni mwa mambo aliyoyatil-ia mkazo Dkt. Majuva ni umuhimu wa kutumia mali kwa manufaa ya wengine, akirejea kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: “Muaminini Allah na Mtume wake; na toeni katika vile alivyokufanyeni nyinyi kuwa ni waangalizi wake...” [Qur'an, 57:7].

Alieleza kuwa zaka husaidia pia kugawa mali katika jamii, kupunguza ulimbikizaji wa mali, kuimarisha ujumuishi wa kijamii na kuwaweza sha wahitaji kujikwamua kiuchumi.

Kwa kuwa ibada zote ambazo Muislamu anawajibika kuzifanya zinatokana na maagizo ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake (rehema na amani iwe juu yake), ibada ya zaka nayo inapaswa kupewa kipaumbele.

Hii ni kwa sababu zaka ni miongoni mwa ibada za wajibu kwa Waislamu waliotim-

iza masharti yake. Kwa msingi huo, elimu kuhusu zaka inapaswa kupewa nafasi kubwa zaidi katika jamii ya Kiislamu.

Uelewa mpana kuhusu zaka utawasaidia Waislamu kufahamu wajibu wao na kutekeleza ibada hiyo kwa usahihi, huku pia wakichangia kupunguza changamoto za kijamii na kiuchumi zinazowakabili.

Tunaipongeza kwa dhati Baitulmaal Tanzania kwa kuona umuhimu wa kueneza elimu ya zaka mikoani. Pamoja na pongezi zetu hizo, tunashauri kuwepo kwa uwazi katika ukusanyaji wa zaka ili kujenga uaminifu miongoni mwa Waislamu na kuhakikisha inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Waislamu wanapopata taarifa sahihi kuhusu kiasi cha zaka kina- chokusanywa, namna kinavyogawanywa na matokeo yanayopatikana kwa walengwa, hujenga imani na kuhamasika zaidi kutoa zaka.

Mwisho, tunatoa wito kwa Masheikh, wanazuoni, taasisi na wadau wengine kuunga mkono juhudi hizi kwa kuendelea kutoa elimu kuhusu zaka kupitia majukwaa mbalimbali, yakiwamo misikiti, vyombo vya habari, taasisi za elimu na mitandao ya kijamii.



Afyais natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED

P.O. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe 11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email: info@watercomtz.com





SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Zaka ya Madeni inatolewaje?

Swali: Mtu ameugua ugonjwa wa Ukimwi (AIDS), na madaktari wametabiri kwamba muda wake wa kuishi katika maisha haya ni mfupi sana. Je, hukumu ya kutubu kwake katika wakati huu iko-je?

Jibu: Anapaswa kuharakisha kutubu, hata kama ni katika dakika za mwisho za maisha yake. Hii ni kwa sababu mlango wa toba uko wazi, kwa vyovyote vile, maadamu akili yake bado iko timamu.

Si kutubu tu, anapaswa pia kujiepusha na maasi. Hii ni kwa sababu muda wa maisha uko mikononi mwa Allah, na henda makadirio yao yakawa si sahihi, akawa anaishi kwa muda mrefu zaidi. Kwa hali yoyote ile, ni wajibu kwake kuharakisha kutubu na awe mkweli katika toba yake, ili Allah amkubalie toba yake.

Allah Mtukufu anasema katika Qur'an: "Na tubuni kwa Allah nyote, enyi Waumini, ili mpate

kufaulu." [24:31]. Na kauli Yake: "Na hakika Mimi ni Mwingi wa kusamehe kwa mwenye kutubu, akaamini, akatenda mema, kisha akaongoka." [Qur'an, 20:82].

Pia, hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume wa Allah (Allah amshushie rehema na amani): "Hakika Allah huikubali toba ya mja maadamu hajafikia hali ya kukaribia kukata roho." Yaani, maadamu mtu hajafikia hali ya kukata roho na kupoteza fahamu zake. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Swali: Zaka ya madeni inatolewaje?

Jibu: Madeni yanahusiana na hukumu za zaka kwa namna tofauti, kutegemea uwezekano wa deni kulipwa, chanzo chake na muda ambao mdai amelipokea. Kwa mujibu wa swali hukumu zake ni kama ifuatavyo:

Vigawanyo:

Madeni yanagawanyika katika sehemu kuu mbili. Kwanza, deni ambalo halitarajiwa kulipwa na deni ambalo linatarajiwa

kulipwa.

Hukumu ya zaka ya deni lisilotarajiwa kulipwa:

Deni ambalo halitarajiwa kulipwa kwa sababu yoyote ile, zaka yake haitakuwa wajibu kwa mdai katika kipindi ambacho hana matumaini ya kulipata.

Hata hivyo, ikiwa mdai atalipwa pesa zake baadaye, atanza kuhesabu mwaka kuanzia siku alipolipokea. Mwaka mmoja kamili unapopita, zaka yake itakuwa wajibu.

Hukumu ya zaka ya deni ambalo mdaiwa analichelewesha kulipa:

Ikiwa mdaiwa anachelewesha kulipa deni licha ya mdai kumtaka alilipe, mpaka mdai akate tamaa ya kulipata, basi zaka ya deni hilo haitakuwa wajibu kwa mdai katika kipindi hicho.

Ikiwa baadaye atafanikiwa kulipata deni hilo, zaka yake itakuwa wajibu baada ya kupita mwaka mmoja kamili tangu siku alipolipokea. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Sitisho la vita labaki kwenye karatasi Gaza

Zaidi ya mashirika 100 ya kimataifa ya misaada na haki za binadamu yamesema makubaliano ya kusitisha vita katika Ukanda wa Gaza yameshindwa kuwaletea usalama Wapalestina, huku mauaji, njaa na vikwazo vya misaada vikiendelea mwaka mmoja tangu makubaliano hayo yafikiwe Oktoba 10, 2025.

Katika taarifa ya pamoja iliyotolewa Oktoba 9, mashirika hayo, yakiwemo Amnesty International, Save the Children, Oxfam na Norwegian Refugee Council, yamesema zaidi ya Wapalestina 1,400, wakiwemo watoto wasiopungua 327, wameuawa katika mashambulizi ya Israel tangu kutangazwa kwa makubaliano hayo yaliyofikiwa kwa ushawishi wa Marekani.

Wakati hali hiyo ikiendelea, takwimu za Wizara ya Afya ya Palestina zinaonesha zaidi ya Wapalestina 74,000 wameuawa tangu vita vilipoanza Oktoba 2023, huku zaidi ya wagonjwa 18,500, wakiwemo watoto 4,000, wakihitaji kuhamishiwa nje ya Gaza kwa matibabu maalumu.

Aidha, takribani watu milioni 1.4

wanakabiliwa na kiwango kikubwa cha uhaba wa chakula, wakati asilimia 80 ya majengo katika eneo hilo yameharibiwa. Mashirika hayo yamesema vikwazo vya kuingiza vifaa vya ujenzi, dawa na misaada vinaendelea kukwamisha juhudi za kurejesha maisha ya kawaida.

Katibu Mkuu wa Norwegian Refugee Council, Jan Egeland, amesema inasikitisha kuwa mwaka mmoja baada ya makubaliano, hali ya Wapalestina haijabadilika kwa kiwango kinachotarajiwa. Mashirika hayo yametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuhakikisha makubaliano yanatekelezwa, raia wanalindwa na wahusika wa ukiukaji wa haki za binadamu wanawajibishwa.





Uislamu wawa kisingizio cha mrengo wa kulia maandamano Ufaransa

Maandamano makubwa ya wanafunzi nchini Ufaransa yameingia katika mjadala wa kisiasa kuhusu Uislamu na uhamiaji, huku baadhi ya wanasiasa wa mrengo wa kulia wakiyatumia kukosoa sera za uhamiaji.

Miongoni mwao ni Rais wa Marekani, Donald Trump, ambaye Oktoba 6, 2026, alidai kuwa maandamano hayo hayatokani na matatizo ya elimu, bali ongezeko la wahamiaji na kile alichokiita juhudi za Uislamu kuitawala Ufaransa.

Kupitia mtandao wake wa Truth Social, Trump alisema kinachoendelea Ufaransa ni matokeo ya uhamiaji mkubwa usiodhibitiwa, akidai kuwa suala hilo halihusu shule.

Hata hivyo, madai hayo ya uongo hayajaunga mkono na ushahidi wowote.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Ufaransa, maandamano yalianza Septemba 21 katika eneo la Créteil, karibu na Paris, baada ya wanafunzi na walimu kulalamikia uhaba wa

walimu, msongamano madarasani na uchakavu wa majengo ya shule. Maandamano yameenea katika miji mbalimbali, huku Serikali ya Rais Emmanuel Macron ikiahidi kuongeza walimu 3,000 katika shule zilizoathirika.

Kauli ya Trump imeibua mjadala kuhusu namna masuala ya Uislamu na uhamiaji yana-vyohusishwa na matatizo ya kijamii nchini Ufaransa, licha ya madai ya waandamanaji kujikita katika kuboresha elimu.

Chuki dhidi ya Waislamu yaongezeka kwa asilimia 15 Uingereza

LONDON. Vitendo vya uhalifu vinavyochochewa na chuki dhidi ya Waislamu nchini Uingereza vimeongezeka kwa asilimia 15, huku Waislamu wakiendelea kuwa kundi la kidini linalolengwa zaidi kwa idadi ya matukio, kwa

mujibu wa takwimu mpya za Serikali.

Takwimu zilizotolewa mwishoni mwa wiki na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Uingereza zinaonyesha kuwa polisi walirekodi matukio 5,132 ya uhalifu wa chuki dhidi ya Waislamu katika England na Wales kwa mwaka ulioishia Machi 2026, ikilinganishwa na matukio 4,479 mwaka uliotangulia.

Matukio hayo yanawakilisha takribani asilimia 45 ya makosa 11,419 ya chuki za kidini yaliyorekodiwa katika kipindi hicho.

Kwa ujumla, makosa yote ya chuki yalifikia 146,825, ongezeko la asilimia saba, huku yale

yaliyohusiana na chuki za kidini yakiongezeka kwa asilimia 13. Ripoti hiyo imehusisha ongezeko la baadhi ya matukio na maandamano yenye vurugu pamoja na migogoro ya kimataifa. Hata hivyo, Wayahudi walikabiliwa na kiwango kikubwa zaidi cha matukio kwa kulinganisha na idadi yao ya watu.

Waziri anayeshughulikia masuala ya polisi, Sarah Jones, alisema Serikali haitavumilia vitisho na ukatili unaowalenga watu kutokana na utambulisho wao.

Serikali imeahidi kuimarisha ulinzi wa jamii na maeneo ya ibada.



Haki na wajibu wa mke aliye katika eda

Maisha ya ndoa ni msingi mkuu katika kujenga familia na jamii. Ni miongoni mwa malengo muhimu ya sheria ya Kiislamu, kwani ndani yake kuna kuen-deleza kizazi pamoja na kulinda nasaba na maumbile ya kibinadamu. Kwa sababu hiyo, hukumu za sheria ya Kiislamu zinazohusu ujenzi wa familia, maisha ya ndoa na jamii kwa ujumla, pamoja na haki, wajibu na majukumu yanayotokana na familia zimeelezwa kwa kina. Lengo ni kuwawezesha watu kutambua kilicho halali na kilicho haramu.

Haki na wajibu wa mke aliye katika eda

Maisha ya ndoa ni msingi mkuu katika kujenga familia na jamii. Ni miongoni mwa malengo muhimu ya sheria ya Kiislamu, kwani ndani yake kuna kuendeleza kizazi pamoja na kulinda nasaba na maumbile ya kibinadamu.

Kwa sababu hiyo, hukumu za sheria ya Kiislamu zinazohusu ujenzi wa familia, maisha ya ndoa na jamii kwa ujumla, pamoja na haki, wajibu na majukumu yanayotokana na familia zimeelezwa kwa kina. Lengoni ni kuwawezesha watu kutambua kilicho halali na kilicho haramu.

Aidha, kifo cha mume na athari zake kwa mwanamke aliyefiwa, iwe ni katika masuala ya mali, ibada au uhusiano na wengine, ni jambo muhimu sana ambalo kila mwanamke kwa namna ya pekee, na kila Muislamu kwa ujumla anapaswa kulijua.

Watu wengi, hasa wanawake waliopoteza waume zao huingia katika makosa ya kisharia yanayohusiana na hukumu za eda. Kwa upande mwingine, kuna baadhi ya wanawake wanaozidisha mipaka katika kufuata hukumu za eda, hasa zile zinazohusiana na maombolezo.

Wengine hufanya mambo yaliyo halali kuwa haramu kwa kudhani kuwa hayaruhusiwi, kama vile kutotoka kabisa nje, kutomsalimia mtu yeyote, au kuacha kabisa kazi na shughuli za kila siku.

Vilevile, kuna wanawake wengi wanaopuuzia kwa kiasi kikubwa kufuata hukumu hizi, iwe kwa kujua au kwa kutokujua, hasa katika masuala ya maombolezo. Huko ni kupindukia katika mambo ambayo hayajaamrisha na sharia.

Maana ya eda

Neno eda, katika lugha ya Kiarabu limeitwa hivi kwa sababu linahusisha kuhesabu vipindi fulani, kama siku za hedhi au miezi.

Katika muktadha wa sheria ya Kiislamu, wanazuoni wa madhehebu ya Shafi'i wanafasiri eda kuwa ni kipindi ambacho mwanamke anapaswa kusubiri ili kubaini iwapo ana ujauzito, au kwa ajili ya ibada ya kumtii Allah, au kutokana na huzuni na majonzi ya kufiwa na mume wake.

Eda inakuwa wajibu kwa mwanamke pale wanandoa wanapotengana baada ya kuingiliana, iwe kwa talaka, kuvunjika kwa ndoa au kuapizana (li'an). Allah anasema: "Na wanawake walioachwa wangoje peke yao mpaka twahara (au hedhi) tatu zipite..." [Qur'an, 2:228].

Pia amesema: "Na wale waliokoma hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mna shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi. Na wenye mimba eda yao mpaka watakapozaa..." [Qur'an, 65:4].

Kukaa eda ni wajibu kwa mwanamke aliyefiwa na mume wake, iwe kifo hicho kimepokea kabla au baada ya kuingiliana naye, kwa mujibu wa kauli ya Allah: "Na wale wanaokufa miongoni mwenu na wakaacha wake, hao wake wangoje peke yao (kwa kukaa eda) miezi minne na siku kumi..." [Qur'an, 2:234].

Ama ikiwa ndoa imefungwa kisha mume akamwacha mke kabla ya kumuingilia, basi mwanamke hana eda, kwa kauli ya Allah: "Enyi mliaoamini! Mki-oa wanawake Waumini kisha mkawaacha kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayoihesabu..." [Qur'an, 33:49].

Eda imewekwa kwa hekima na maana nyingi muhimu. Miongoni mwa hekima hizo ni kuhakiki-

sha kuwa mwanamke hana ujauzito ili kuepuka kuchanganyika kwa nasaba. Pia, eda huonesha uzito na heshima ya mkataba wa ndoa na kuuthamini.

Vilevile, eda humpa mume nafasi ya kutafakari upya uamuzi wake katika talaka ya kurejea, na huenda akarejea kwa mkewe ndani ya muda huo. Pia, eda huonesha haki ya mume na athari za kuondoka kwake kwa kumzuia mwanamke kujipamba wakati wa eda ya kifo.

Ndiyo maana eda ya kifo ina uzito mkubwa zaidi kuliko huzuni inayotokana na kufiwa na wazazi au watoto. Aidha, eda inalenga kulinda haki za mume, maslahi ya mke na haki za mtoto, pamoja na kutekeleza amri ya Allah ya kuweka eda.

Allah anasema: "Haiwi kwa Muumini mwanaume wala Muumini mwanamke kuwa na hiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi." [Qur'an, 33:36].

Eda kwa mwanaume

Swali linazuka: Je, mwanaume naye ana eda? Jibu ni kuwa eda haimlazimu mwanaume. Anaweza kuoa mwanamke mwingine mara baada ya kuachana na mke wake bila kusubiri eda ya mke aliyemwacha kumalizika.

Hata hivyo, kuna hali ambazo hulazimika kusubiri, si kwa maana ya eda, bali kwa sababu ya vikwazo vya kisharia. Mfano, ikiwa anataka kumuoa dada wa mke aliyemwacha, au shangazi yake, au yeyote ambaye hairuhusiwi kuwaoa kwa pamoja.

Pia ikiwa ameacha mke wa nne na anataka kuoa mwingine, atalazimika kusubiri eda ya talaka rejea imalizike. Ama katika talaka isiyo ya kurejea, Jopo la wanazuoni linaona kuwa halazimiki kusubiri. Hivyo, kuzuiwa kwa mwanaume kuoa katika hali hizi hakuitwi eda, iwe kwa maana ya kilugha au ya kisharia.

Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah



Afyais natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED

P.O. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe 11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email: info@watercomtz.com



HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

NA

**Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383**



Utalii halali waingia hatua mpya duniani

LONDON. Wadau wa sekta ya utalii halali duniani wametaka nchi na kampuni za utalii kuboresha huduma zinazokidhi mahitaji ya Waislamu, wakisisitiza umuhimu wa kujenga imani ya wasafiri ili kunufaika na soko hilo linalokua.

Wito huo umetolewa Oktoba 10, 2026, kati-

ka Kongamano la London Halal Forum, lililowakutanisha wawekezaji, watunga sera na viongozi wa sekta ya utalii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halal Travel Network, Hafsa Gaher, alisema sekta hiyo imevuka hatua ya kuthibitisha ukubwa wa soko na sasa inapaswa kuzingatia ubora wa hudu-

ma, elimu kwa wahudumu na taarifa sahihi kwa wasafiri. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa CrescentRating na HalalTrip, Fazal Bahardeen, alisema uaminifu wa wasafiri ni msingi wa kuwavutia watalii Waislamu.

Alisisitiza umuhimu wa upatikanaji wa vyakula halali, huduma zinazozingatia mahitaji ya kidini na taarifa za kuaminika wakati wa kufanya nafasi za safari.

Mwakilishi wa Turkish Airlines, Melih Sukru Ecertas, alisema ushirikiano kati ya mashirika ya ndege, hoteli na waandaji wa safari ni muhimu katika kukuza utalii huo.

Kongamano hilo, lililoandaliwana Halal360, lilijadili pia fursa za uwekezaji, teknolojia na biashara katika uchumi wa halal duniani.

Somalia yataka kulin-da misingi ya Sharia katika sheria ya benki

MOGADISHU. Wabunge wa Somalia wametaka marekebisha ya sheria ya Benki Kuu ya nchi hiyo yazingatie misingi ya Sharia, huku wakihoji masharti yanayohusu huduma za benki za Kiislamu, uhuru wa benki hiyo na mipango ya kurejesha noti za sarafu ya taifa.

Hoja hizo ziliibuka wakati Bunge likikamilisha hatua ya pili ya kujadili muswada wa kurekebisha Sheria Na. 130 ya mwaka 2012, Oktoba 10, 2026.

Mbunge Abdullahi Arab alihoji kuondolewa kwa kifungu kilichokuwa kikielekeza benki kuzingatia misingi ya fedha za Kiislamu, akitaka sheria mpya iendane na Sharia.

Alipendekeza pia kuundwa kwa kamati kuu ya usimamizi wa Sharia itakayoshauri Benki Kuu kuhusu miamala na mapato yanayohu-

sisha riba.

Wabunge wengine walihoji uhuru wa Benki Kuu na pendekezo la kiwango cha ubadilishaji cha shilingi 100 za Somalia kwa dola moja ya Marekani, wakitaka msingi wake wa kiu-chumi ufafanuliwe. Aidha, walitaka Serikali kueleza lini noti mpya za shilingi ya Somalia zitaanza kutumika, hatua inayolenga kurahisisha miamala midogo na kupanua huduma za kifedha. Kamati ya Bunge imeahidi kupitia hoja hizo kabla ya muswada kusomwa kwa mara ya tatu. Marekebisha hayo bado hayajawa sheria.

Al Baraka yafadhili kongamano la Sharia Bahrain

MANAMA, BAHRAIN. Kundi la taasisi za fedha za Kiislamu la Al Baraka Group, kwa kushirikiana na benki zake za Misri, Jordan

na Uturuki, limetangaza kuwa mfadhili wa ngazi ya dhahabu wa Kongamano la 24 la Mwaka la Mabaraza ya Sharia linaloandaliwa na AAOIFI.

Kongamano hilo linafanyika Oktoba 11-12, 2026, katika Hoteli ya Crowne Plaza, Manama, kwa msaada wa Benki Kuu ya Bahrain.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Oktoba 11, ufadhili huo unalenga kuunga mkono juhudi za AAOIFI za kuimarisha viwango vya Sharia na taaluma katika sekta ya fedha za Kiislamu duniani.

Kongamano linawakutanisha wanazuoni wa Sharia, wataalamu wa fedha, watafiti na wasimamizi wa sekta hiyo kujadili changamoto za kisheria na kiutendaji.

Mijadala mitano imepangwa, ikihusu ulinganifu wa viwango vya Sharia na sheria za nchi, gharama halisi za ukopesha, mikataba ya ufadhili wa pamoja na athari za mabadiliko ya mazingira katika mikataba ya kifedha.

Al Baraka Group inatoa huduma za benki za Kiislamu kupitia taasisi zake katika nchi 13, ikiwa na mtandao wa matawi zaidi ya 600.

NGUVU YA WAQF:

Yadhamini vijana 25 Ibun Jazar Islamic Schools kujiunga na Albukhari International University

Leo tunachambua kwa kina mfumo wa Waqf na jinsi unavyoweza kubadilisha maisha ya Watanzania, tukirejea udhamini wa vijana 25 kwenda masomoni nje ya nchi.

Huu ni mlinganyo wa umma unaotaka kusimama: Wahyi unaotoka kwa mahafidh wa Qur'an kutoka kituo cha Ibn Jazar na elimu inayokwenda kutafutwa ugenini katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Albukhary (AIU) nchini Malaysia.

Jinsi mfumo wa Waqf unavyofanya kazi

Mzunguko wa kudumu wa fedha na endelevu wa Waqf unajengwa kupitia utoaji wa mtaji wa awali kama waqf wa milele, uwekezaji halali kwenye biashara au miundombinu, uzalishaji wa faida inayofadhili elimu, na uendelevu wa milele wa vizazi hadi vizazi.

Taasisi ya Albukhary inamiliki mali kubwa zilizowekwa kama Waqf nchini Malaysia, zikiwemo Jumba la Makumbusho ya Sanaa ya Kiislamu, majengo ya ghorofa, na vituo vya ununuzi. Mali hizi zinazalisha mapato endelevu kupitia ukodishaji na biashara mbalimbali.

Mbali na Waqf, taasisi pia huongezea fedha za Zakat kutoka kwa kampuni zake na wakati mwingine mchango wa kibinafsi kutoka kwa utajiri wa mwanahisani Tan Sri Syed Mokhtar Albukhary, huku Waqf ikiwa ndio uti wa mgongo na chanzo cha uhakika cha milele.

Kuhusu Tan Sri Syed Mokhtar Albukhary, huyu ni mmoja wa wafanyabiashara na wafadhili mashuhuri nchini Malaysia, ambaye licha

ya kuanza maisha kwa unyonge na kushindwa kumaliza shule ya upili, amejenga himaya kubwa ya kibiashara inayojumuisha sekta za usafirishaji, magari, na miundombinu.

Kupitia taasisi aliyoiasisi ya Albukhary (Albukhary Foundation), amejitolea kwa hali na mali kusaidia jamii ambapo katika sekta ya elimu, amefanya mapinduzi makubwa kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Albukhary (AIU) kinachotoa ufadhili kamili wa masomo (scholarships) kwa wanafunzi wasiojiweza kutoka mataifa zaidi ya 40 duniani, akiamini kuwa elimu ndiyo silaha kuu ya kujikwamua kutoka kwenye umaskini.

Nyayo za kihistoria: vyuo vikuu vya awali vilivyojengwa kwa Waqf

Ili kuelewa nguvu ya mfumo usioweza kuingiliwa na siasa, ni muhimu kuangalia vyuo vikuu vya kihistoria vya Kiislamu vilivyoendeshwa kabisa na Waqf:

Hii hapa orodha iliyopanuliwa zaidi kwa kuongeza vyuo vikuu na madrasah nyingine maarufu za kihistoria ambazo nazo zilianzishwa au kuendeshwa kwa mfumo wa Waqf, pamoja na kutoa maelezo yaliyopanuka kwa kina zaidi:

Mosi, Chuo Kikuu cha Ez-Zitouna – Tunisia
Chuo hiki kilianzishwa karibu mwaka 737 Miladia (karne ya nane) mjini Tunis, Tunisia, wakati wa Dola ya Umayyad, kwa mchango wa viongozi wa eneo hilo Mali na ardhi zilizotolewa kama waqf zilitumika kugharamia walimu, uendeshaji wa msikiti na chuo, pamoja na huduma kwa wanafunzi.

Ez-Zitouna ni miongoni mwa vyuo vikuu vya zamani zaidi duniani na kituo kikubwa cha elimu ya Kiislamu na sayansi Afrika Kaskazini. Miongoni mwa wahitimu wake maarufu ni mwanahistoria Ibn Khaldun.

Pili, Chuo Kikuu cha Al-Qarawiyyin –

Morocco

Chuo hiki kilianzishwa mwaka 859 Miladia katika mji wa Fez, Morocco, na Fatima al-Fihri. Kwa mujibu wa maelezo yaliyowasilishwa, Fatima al-Fihri alitenga urithi wake wote kama waqf kwa ajili ya kuendesha taasisi hiyo, kujenga nyumba za walimu na kutoa elimu bila malipo.

Chuo hicho kinatambuliwa na UNESCO na Guinness World Records kama mojawapo ya taasisi kongwe zaidi za elimu ya juu duniani zinazoendelea kufanya kazi bila kukatika tangu kuanzishwa kwake. Tukio la vijana wa Ibn Jazar linakumbusha historia ya Fatima al-Fihri, ambaye alitumia urithi wake wote kama Waqf kwa ajili ya kuanzisha taasisi ya elimu.

Tatu, Chuo Kikuu cha Al-Azhar – Misri

Chuo cha Al-Azhar kilianzishwa mwaka 975 Miladia mjini Cairo, Misri, chini ya utawala wa Usultani wa Fatimid. Mali kubwa za waqf, zikiwamo ardhi za kilimo na masoko, zilitumika kugharamia elimu, chakula, posho za wanafunzi na mishahara ya walimu.

Al-Azhar kilikuwa kituo kikuu cha taaluma za Kiislamu na sayansi katika ulimwengu wa Kiarabu. Kimeendelea kuwa na ushawishi mkubwa wa kisomo duniani.

Nne, Madrasah ya Sankore – Mali

Madrasah ya Sankore, inayojulikana pia kama Sankore University, ilianzishwa katika mji wa Timbuktu, Mali, katika karne ya 10, ingawa ilistawi zaidi kati ya karne ya 14 na 16. Taasisi hiyo ilianzishwa na kuendelezwa kwa juhudi za jamii ya eneo hilo, wafanyabiashara matajiri na viongozi mbalimbali, akiwamo Mansa Musa. Mali za waqf zilizotolewa na wafanyabiashara matajiri zilihakikisha upatikanaji wa maktaba kubwa, mishahara ya walimu na chakula cha bure kwa wanafunzi. Sankore ilikuwa kituo kikubwa cha elimu ya juu Afrika Magharibi, kilichohifadhi maelfu ya maandishi ya sayansi, hesabu, sheria na elimu ya dini. Kilikuwa na uwezo wa kukusanya wanafunzi na wanazuoni kutoka maeneo mbalimbali.

Tano, Madrasah ya Al-Nizamiyya – Iraq

Madrasah ya Al-Nizamiyya ilianzishwa mwaka 1065 Miladia mjini Baghdad, Iraq, na Nizam al-Mulk, aliyekuwa Waziri wa Dola ya Seljuk. Taasisi hiyo ilifadhiliwa kikamilifu kupitia mfumo wa waqf wa serikali, uliotoa elimu, malazi na ruzuku za kifedha kwa wanafunzi bila malipo.



Usisubiri uwe tajiri kuandika wosia

Watu wengi hudhani kwamba kuandika wosia ni jambo linalowahusu matajiri wenye nyumba, mashamba, magari na fedha nyingi benki. Hata hivyo, katika Uislamu, wosia si suala la utajiri pekee, bali ni njia muhimu ya kulinda haki za watu, kutimiza wajibu na kuzuia migogoro inayoweza kutokea baada ya kifo.

Fikiria mtu anayefariki dunia akiwa na kiwanja kidogo, fedha alizokopa kwa rafiki, mali aliyokabidhiwa na jirani au akiba katika simu yake. Ikiwa hakuna anayefahamu mambo hayo, nini kitatokea baada ya kifo chake? Huenda madeni yake yasilipwe, mali za wengine zikachanganywa na urithi wake au familia ikaingia katika migogoro ambayo ingeweza kuepukika. Hii ndiyo sababu Uislamu unahimiza Muislamu kuweka wazi haki na wajibu wake kabla hajafariki dunia, bila kujali ukubwa wa mali anayomiliki. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema katika Hadith iliyopokewa na Abdullah bin Umar (Allah amridhie) kwamba si jambo linalofaa kwa Muislamu mwenye jambo la kuusia kupitisha siku mbili bila kuwa na wosia wake ulioandikwa. Hadith hii imepokewa na Bukhari, namba 2738, na Muslim, namba 1627. Mafundisho haya yanatukumbusha kwamba kifo hakina ratiba na kwamba maandalizi ya kulinda haki za wengine hayapaswi kuahirishwa.

LAKINI WOSIA NI NINI HASA?

Kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu, wosia ni maelekezo anayoyaaacha mtu kuhusu mambo halali yanayopaswa kutekelezwa baada ya kifo chake. Maelekezo hayo yanaweza kujumuisha taarifa za madeni, mali alizokabidhiwa, haki anazodai kwa wengine, namna ya kushughulikia mazishi yake na mali anayotaka kuitoa

kwa watu au shughuli za kheri kwa mujibu wa Sharia.

Kwa mfano, mfanyabiashara mdogo anaweza kuandika kwamba anadaiwa fedha na watu fulani au kwamba kuna mali za wateja ambazo hazipaswi kuhesabiwa kuwa zake. Vilevile, mzazi anaweza kuweka maelekezo kuhusu mtu anayempendekeza kusimamia malezi ya watoto wake wadogo, kwa kuzingatia Sharia na sheria za nchi.

Hata hivyo, jambo muhimu ni kutofautisha wosia na mirathi.

Mirathi ni haki ya warithi iliyowekwa na Allah, wakati wosia unahusu mambo ambayo mtu ameruhusiwa kuyaelekeza yatekelezwe baada ya kifo chake.

Allah ameeleza mgawanyo wa mirathi katika Qur'an [4:11-12]. Kwa hiyo, mtu hawezi kutumia wosia kumnyima mrithi halali haki yake kwa sababu ya chuki, ugomvi au upendeleo.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ameeleza kwamba Allah amempa kila mwenye haki haki yake, hivyo hakuna wosia wa kumpa mrithi sehemu ya ziada, kwa mujibu wa kanuni ya jumla ya Sharia. Aidha, mtu mwenye warithi anaruhusiwa kuusia sehemu isiyoziidi theluthi moja ya mali inayobaki baada ya kutimiza haki na madeni yanayotangulia wosia, kwa watu wasio warithi au shughuli halali za kheri.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alipomuongoza Swahaba Sa'd bin Abi Waqqas (Allah amridhie), alieleza kwamba theluthi moja inatosha, tena ni nyingi, akisisitiza umuhimu wa kutowaacha warithi katika umasikini.

Wosia pia ni fursa ya kuacha kheri itakayoendelea kuwanufaisha wengine hata baada ya kifo.

Katika makala iliyochapishwa na shirika la misaada la Oxfam, Machi 18, 2025, mtaalamu wa sheria za wosia za Kiislamu, Yasmin Hoque, anaeleza kwamba wosia si utaratibu wa kugawa mali pekee, bali pia ni njia ya kuacha urithi wa matendo mema kupitia sadaka jariya.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema kwamba mwanadamu anapofariki, matendo yake hukatika isipokuwa matatu: sadaka yenye kuendelea, elimu yenye manufaa na mtoto mwema anayemuomba dua. Hadith hii imepokewa na Muslim, namba 1631.

Kwa hiyo, mtu anaweza kuusia sehemu inayoruhusiwa ya mali yake kusaidia elimu, kuchimba kisima au shughuli nyingine za kheri zenye manufaa ya kudumu. Hivyo, wosia si njia ya kuwanyima watoto, mke, mume au warithi wengine mali yao, bali ni utaratibu wa kuhakikisha haki zote zinaheshimiwa, huku ukitoa fursa ya kuendeleza kheri.

Kuandika wosia pia husaidia kupunguza migogoro ya kifamilia. Mara nyingi baada ya kifo, ndugu hugombania mali kwa sababu hawajui marehemu alikuwa anamiliki nini, anadaiwa kiasi gani au alikuwa amekabidhiwa mali gani.

Kwa hiyo, Muislamu anaweza kuanza kwa kuorodhesha mali zake, madeni, nyaraka muhimu na haki za wengine. Kisha achague mtu mwaminifu, mwenye uwezo na uelewa wa kutosha, wa kusimamia utekelezaji wa wosia na kushughulikia masuala ya mali kwa mujibu wa Sharia na sheria.

Ni vizuri pia familia au watu wanaohusika kufahamishwa kuhusu uwepo wa wosia na mahali ulipohifadhiwa. Hatua hii inaweza kuzuia mkanganyiko na kurahisisha utekelezaji wake baada ya kifo.

Ni muhimu pia wosia kuandaliwa kwa kuzingatia Sharia na sheria za nchi. Nchini Tanzania, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) hutoa huduma za uandaaji na utunzaji wa wosia. Ushauri wa mwanazuoni mwenye uelewa wa mirathi pamoja na mtaalamu wa sheria unaweza kusaidia kuepusha makosa.

Wosia unapaswa kuwa wazi, wenye taarifa sahihi, tarehe na uthibitisho unaotakiwa kisheeria. Unaweza pia kurekebisha kadiri mazingira yanavyobadilika, kwa mfano baada ya ndoa, kupata watoto au kuongezeka kwa mali na madeni.

Jambo la msingi ni kwamba wosia hauandikwi kwa sababu mtu anatarajia kufa kesho, bali kwa sababu anajua kwamba siku moja atondoka na kuacha nyuma haki za watu zinazopaswa kuheshimiwa.

Hivyo, usisubiri uwe tajiri ndipo uandike wosia. Hata mali ndogo na deni dogo vinaweza kuwa sababu ya kuwajibika mbele ya Allah. Wosia mzuri si kipimo cha utajiri wa mtu, bali ni ushahidi wa uadilifu, uaminifu na kujali haki za wengine.

Matumizi ya Akili Unde kwa mtazamo wa Kiislamu



Katika dunia inayobadilishwa kwa kasi na Akili Unde (AI), Waislamu wanakabiliwa na swali muhimu: Je, teknolojia hii inaruhusiwa katika Uislamu au inapingana na mafundisho yake? Jibu linahitaji ufahamu wa teknolojia, misingi ya Qur'an na Sunna, pamoja na matumizi yenye uwajibikaji.

Matumizi ya Akili Unde kwa mtazamo wa Kiislamu

Akili Unde ni istilahi inayotumika kuelezea teknolojia, maarufu kwa kifupi kama AI, inayotumia mfano wa akili ya binadamu katika mashine. Ni tawi la sayansi ya kompyuta linalohusisha kujenga mifumo na programu zinazotambua mazingira yao na kutenda ipasavyo.

Teknolojia hii mpya inazidi kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku, huku sekta ya AI duniani ikitarajiwa kukua kwa kiasi kikubwa katika miaka ijayo. Kwa maana hiyo, hakuna Muislamu anayeweza kuepuka athari za Akili Unde.

Hakuna ushahidi wa wazi unaonesha kuwa mafundisho ya Kiislamu yanakataza matumizi ya Akili Unde au yanazuia kabisa teknolojia hiyo. Badala yake, Qur'an inawahimiza watu kutumia rasilimali walizopewa kwa namna yenye manufaa katika maisha yao.

Allah anasema: “Na amefanya vikutumiki- eni vilivyomo mbinguni na vilivyomo kati- ka ardhi, vyote vimetoka kwake.” [Qur'an, 45:13]. Hivyo basi, matumizi ya AI yamekuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku.

Unapouliza swali kupitia ChatGPT, Ramani za Google zinapokuelekeza unakokwenda, Netflix inapokupendekezea filamu au kipindi cha kutazama, au benki yako inapogundua jaribio la udanganyifu, yote hayo ni mifano ya matumizi ya Akili Unde.

AI imeingia kimya kimya katika kila kona ya maisha yetu. Hivi sasa, Waislamu duni- ani kote wanajiuliza swali lilelile la dharura: Je, matumizi ya AI ni halali au haramu? Je,

ninaweza kuitumia? Je, ninapaswa kuiogo- pa? Na kama Muislamu, ninawezaje kuishi na teknolojia hii na kuitumia kwa usahihi?

Makala hii inalenga kutoa majibu ya kina na yaliyo wazi kwa kuzingatia misingi ya Qur'an na Sunna pamoja na fat-wa za wanazuoni wa Kiislamu wa zama hizi.

AI ni ishara ya Ukuu na Utukufu wa Mwenyezi Mungu

Teknolojia mpya zinazoibuka kila zama ni miongoni mwa ishara zinazoonesha Ukubwa na Utukufu wa Mwenyezi Mungu, Muumba wa mwanadamu: “Amemfundisha mwan- adamu mambo mengi asiyoyajua.” [Qur'an, 96:5].

Kimsingi, Uislamu haupingani na teknolo- jia, wala haujawahi kuwa hivyo. Dini ya Kiis- lamu haikatazi uvumbuzi wala matumizi ya teknolojia mpya. Wanazuoni wakubwa, akiwamo Ibn Taymiyyah (Allah amrehemu) wameweka kanuni muhimu katika sheria ya Kiislamu inayohusiana na mambo ya dunia na uvumbuzi mpya.

Kanuni ya msingi ya fiqhi kuhusu mambo mapya inasema: “Vitu vyote vipya ni safi na vinaruhusiwa, isipokuwa pale vinapopingana na sheria tukufu ya Mwenyezi Mungu.” [Ibn Taymiyyah]. Hii ndiyo kanuni ya msingi inayotumika katika Uislamu.

AI yenyewe si halali wala haramu. Ni chom- bo au nyenzo, na hukumu yake inategemea namna inavyotumika. Ni sawa na kisu, amba- cho kinaweza kutumika kuandaa chakula au kusababisha madhara. Hivyo, matumizi yake

ndiyo huamua ikiwa ni halali au haramu.

Kwa karne nyingi, Waislamu wamekuwa wakikabiliana na teknolojia mpya zilizoibu- ka katika kila zama, zikiwamo mashine za uchapishaji, upigaji picha, redio, televisheni, simu na intaneti.

Kila teknolojia mpya imewahi kuibua mjadala miongoni mwa wanazuoni kabla ya kutolewa kwa hukumu kuhusu matumizi yake. AI nayo haina tofauti; inapitia mchaka- to huohuo wa kutathminiwa kwa kuzingatia misingi ya Kiislamu.

Maana halisi ya AI

Kabla ya kuitathmini Akili Unde (AI) kwa mtazamo wa Kiislamu, ni muhimu kwanza kuelewa AI ni nini hasa. Waislamu wengi bado wana dhana potofu kuhusu teknolojia hii, hali ambayo inaweza kusababisha hofu isiyo na msingi au matumizi yasiyofaa.

AI si kiumbe hai; haina roho, fahamu, hiari wala chembe hai. Katika mtazamo wa theolo- jia ya Kiislamu, roho ni pumzi ya kimungu inayotolewa kwa viumbe hai pekee. AI ni mfumo wa kihisabati unaochakata mantiki ya uwezekano (probability) katika data.

AI haijui mambo yote

AI inaweza kujua tu kile ilichofundishwa, inaweza kuwa na upendeleo na inaweza kutoa taarifa zinazosikika kuwa za kweli, lakini kumbe ni potofu. AI haijitegemei kama binadamu.

Nyuma ya kila mfumo wa AI kuna binad- amu aliyeubuni, akaufundisha na kuamua jinsi utakavyotumika. Kwa hiyo, wajibu wa kimaadili unabaki kwa binadamu, si kwa mashine iliyoundwa. AI ni chombo kama zilizvyo zana nyingine zote, na uhalali wake hutegemea madhumuni na namna kinavyo- tumika.

Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah





Twisheni sawa, lakini zisiwanyime watoto haki ya kwenda madrasa

Katika zama hizi ambazo wazazi na walezi wengi wanahangaika kuwatafutia watoto wao shule bora, masomo ya ziada na ujuzi wa lugha, kuna swali muhimu la kujiuliza: Tumeiweka wapi madrasa katika maisha ya watoto wetu? Kupitia madrasa, watoto hujifunza kusoma Qur'an, Sunna za Mtume Muhammad, misingi ya ibada, adabu, dua na maadili ya Kiislamu. Hata hivyo, kadiri muda wa kukaa shuleni unavyoongezeka, baadhi ya watoto hukosa kabisa muda wa kwenda madrasa, huku baadhi ya wazazi wakiona elimu ya dini kuwa si muhimu katika maisha ya mtoto.



Jambo hili halipaswi kupuuzwa, kwa kuwa linaweza kuathiri malezi, mwenendo na mustakabali wa watoto wetu. Mtoto anaposhindwa kwenda madrasa, hapotezi tu fursa ya kujifunza Qur'an, hadith au dua, bali pia hukosa nafasi ya kupata misingi ya maadili na ibada atakazopaswa kufanya katika maisha yake yote.

Madrassa ina nafasi kubwa katika kumjengea mtoto msingi wa kumtambua Muumba wake, kuwaheshimu wazazi na walezi, pamoja na kuishi kwa kuzingatia maadili mema ya dini. Mafunzo anayoyapata mtoto katika umri mdogo yanaweza kuwa mwongozo muhimu katika maisha yake, hasa anapokabiliwa na changamoto, vishawishi na kufanya maamuzi mbalimbali.

Kwa sababu hiyo, wazazi na walezi wanapaswa kutambua kuwa elimu ya dini si jambo la ziada linaloweza kuachwa pindi ratiba ya shule inapokuwa ngumu. Mtoto anayepata elimu ya mazingira sambamba na malezi ya kidini hujengewa msingi mpana wa kuwa mtu mwenye maarifa, nidhamu na uwajibikaji katika jamii.

Nini kifanyike?

Ratiba za masomo ya ziada zinapaswa kupangwa kwa umakini ili zisiwanyime watoto fursa ya kwenda madrasa na kupata elimu ya dini.

Katika hili, wazazi na walimu wana wajibu wa kuhakikisha ratiba za twisheni haziingiliani na

muda wa madrasa. Twisheni ni muhimu katika kukuza maendeleo ya kitaaluma ya mtoto, lakini isiwe sababu ya kumtenga na madrasa.

Ni muhimu shule, wazazi na walezi kushirikiana kupanga ratiba zinazompa mtoto nafasi ya kupata elimu zote mbili bila kumchosha. Ieleweke wazi kuwa Uislamu haujengi ushindani kati ya elimu ya dini na elimu yenye manufaa katika maisha. Mtoto anaweza kuwa mwanafunzi bora wa sayansi, hisabati, lugha au teknolojia na wakati huohuo akawa na msingi mzuri wa dini. Ndiyo maana Qur'an inasisitiza umuhimu wa kusoma na kujifunza.

Katika Surat Al-Alaq (Qur'an 96:1), Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba." Hivyo, mtoto anapopelekwa madrasa, haendi kwa lengo la kuwaondolea wazazi usumbufu wa nyumbani, bali kupata elimu ya dini itakayomsaidia kuishi kwa misingi bora hapa duniani na kujiandaa kwa maisha ya Akhera.

Elimu anayoipata madrasa inapaswa kuungwa mkono na mwenendo wa wazazi nyumbani ili aweze kuona kwa vitendo umuhimu wa yale anayofundishwa. Mzazi anayeswali, anayeheshimu wengine, anayesamehe na anayesema kweli, humfundisha mtoto wake somo lisilosahaulika.

Madrasa ziwe mahali pa kuwavutia watoto

Madrassa inaweza kuwa sehemu ya kuwavutia watoto ikiwa masomo yatawasilishwa kwa mbinu zinazowafanya waone uhusiano kati ya wanachojifunza na maisha yao ya kila siku. Kwa hiyo, mjadala huu unapaswa pia kuhusisha aina ya mafunzo wanayopewa.

Katika dunia ya sasa inayokabiliwa na changamoto ya mmomonyoko wa maadili, tunahitaji watoto wanaojua kusoma na kuandika, lakini pia wanaowaheshimu wazazi wao.

Tunahitaji vijana wanaojua kutumia teknolojia, lakini pia wanaojua mipaka ya maadili. Tunahitaji wataalamu bora, lakini pia wenye huruma, hofu ya Mungu na waaminifu. Haya yote yanahitaji ushirikiano wa karibu kati ya wazazi, walimu wa madrasa na jamii kwa ujumla.



ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Swala ya Janaza: Dua ya mwisho ya umma kwa ndugu yao

SEHEMU YA

9

Siku moja baada ya Swala ya faradhi, Imamu alisimama akasema: “Ndugu zangu, kuna Janaza. Mwenye uwezo asiondoke, tushiriki kumswalia ndugu yetu.”

Baadhi ya watu walibaki, lakini wengi waliinuka na kuondoka. Huenda walikuwa na shughuli muhimu. Huenda hawakujua kuwa walikuwa wanaondoka na kuacha fursa ya ibada yenye malipo makubwa mno.

Hali kama hii hujitokeza mara nyingi katika misikiti yetu. Watu wengi hujua kuswali Swala tano za kila siku, lakini wachache hujua nafasi ya Swala ya Janaza katika Uislamu.

Swala ya Janaza Ni faradhi kifayah

Wanazuoni wamekubaliana kwamba Swala ya Janaza ni faradhi kifayah. Ikiwa kundi la Waislamu litaiswali, wengine huondokewa na wajibu. Lakini ikiwa hakuna atakayemswalia Muislamu aliyefariki bila udhuru wa Kisharia, jamii hubeba dhambi kwa kuacha haki ya ndugu yao.

Hivyo, Swala ya Janaza si ibada ya hiari tu, bali ni wajibu wa kijamii ambao unaonesha mshikamano wa Umma.

Kwa Nini Inaitwa Swala ya Janaza?

Tofauti na Swala nyingine, Swala ya Janaza haina rukuu wala sijda. Msingi wake ni kumtukuza Allah, kumswalia Mtume (Allah amshushie rehema na amani), kumuomba dua marehemu na kuhitimisha kwa kutoa salamu.

Kwa hiyo, lengo lake kuu si vitendo vya mwili, bali ni dua na maombezi kwa aliyefariki.

Fadhila ya kushiriki janaza

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Mwenye kuhudhuria Janaza mpaka akaliswalia atapata Qirat moja, na mwenye kuhudhuria mpaka azikwe atapata Qirat mbili.”

Swahaba wakauliza: “Qirat mbili ni kiasi gani?” Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akajibu: “Kama milima miwili mikubwa.” [Bukhari na Muslim].

Hadithi hii inaonesha kuwa kushiriki sala ya janaza si kupoteza muda, bali ni ibada yenye malipo makubwa sana mbele ya Allah.

Namna ya kuswali swala ya janaza

Swala ya Janaza hujengwa juu ya takbira nne.

Takbira ya kwanza: Baada ya kusema Allahu Akbar, husomwa Surat-ul-Fatihah. Kwa mujibu wa hadithi sahihi kutoka kwa Ibn Abbas (Allah amridhie), kusoma Al-Fatihah katika Swala ya Janaza ni Sunna ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Takbira ya Pili: Baada ya takbira ya pili, husomwa Swala ya Ibrahimiyya, kama ile inayosomwa katika tashahhud ya Swala.

Takbira ya Tatu: Hii ndiyo sehemu muhimu zaidi ya Swala ya Janaza. Hapamswaliji humuombeamarehemu duakwa Ikhlas. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Mnapomswalia maiti, basi muombeeni dua kwa Ikhlas.” [Abu Daud]. Ndiyo maana dua hii ndiyo kiini cha Swala ya Janaza.

Takbira ya Nne: Baada ya takbira ya nne, baadhi ya wanazuoni wamependekeza dua fupi,

kisha hutolewa salamu.

Je, lazima dua iwe kwa Kiarabu?

Asili ni kutumia dua zilizofundishwa na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kwa Kiarabu.

Lakini ikiwa mtu hajui Kiarabu, wanazuoni wengi wameeleza kwamba anaweza kumuomba marehemu kwa lugha anayoelewa, hasa ikiwa hawezi kujifunza dua za Kiarabu kwa wakati huo. Allah anajua yaliyomo moyoni na husikia dua za waja Wake.

Wingi wa wanaomswalia marehemu

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Hakuna Muislamu anayefariki, wakamswalia Waislamu arobaini wasiokuwa wanamshirikisha Allah kwa chochote, isipokuwa Allah atawakubalia maombezi yao kwake.” Imepokewa na Muslim.

Hadithi hii inatuhamasisha kushiriki Janaza na kuomba watu washiriki, si kwa kujionesha, bali ili marehemu apate dua nyingi kutoka kwa Waumini.

Makosa yanayoonekana katika jamii

Baadhi ya makosa yanayojitokeza ni kuongea wakati wa swala ya Janaza, kucheka au kutumia simu wakati wa swala ya Janaza na kudhani kuwa Swala ya Janaza ni kwa ajili ya wazee pekee.

Makosa mengine ni kutowajulisha Waislamu kuhusu Swala ya Janaza kwa hofu ya usumbufu na kadhalika kuswalia Janaza kwa haraka kiasi cha watu kutokuelewa wanachofanya.

Kosa jingine ni kudhani wanawake hawaruhusiwi kabisa kuswalia Janaza, ilhali asili ya hukumu ni kuwa wanaruhusiwa kushiriki Swala ya Janaza. Kinachokatanzwa na wanazuoni zaidi ni suala la kufuatana na msafara hadi makaburini.

Tunajifunza nini?

Swala ya Janaza ni zawadi ya mwisho ambayo Ummahutoakwandugu yao. Marehemu hawezi tena kuongeza amali zake. Lakini anaweza kunufaika kwa dua za Waumini wanaomswalia kwa ikhlasi.

Kwa hiyo, tusiione Swala ya Janaza kama shughuli ya kawaida. Tuione kama ibada ambayo huenda kesho sisi ndio tutahitaji tufanyiwe.

Hitimisho

Kila Janaza tunaloshiriki ni ukumbusho kwamba safari yetu ya duniani ina mwisho. Leo tunamswalia mwenzetu, kesho huenda wengine wakatuswalia sisi.

Ukifa leo, utaacha alama gani?

Kuna swali linalomfuata kila mtu kama kivuli chake, akubali au akatae: Ni nini kitakachobaki nyuma yangu nitakapoondoka duniani? Tunaishi katika zama ambazo watu wanahangaika zaidi na yale yanayoonekana, huku wakisahau jambo muhimu zaidi – urithi (legacy) watakaoacha baada ya kufa.

Wanajenga majukwaa, lakini hawajengi misingi. Wanakusanya wafuasi, lakini hawakusanyi matendo. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anayaelekeza mawazo yetu kwenye jambo la kudumu zaidi: “Hakika Sisi tunawafufua wafu, na tunayaandika wanayoyatanguliza na wanayoyaacha nyuma.” [Qur’an, 36:12].

Ndugu yangu Muislamu, tafakari kwa makini maneno haya ya Mwenyezi Mungu. Si kile tu ulichokitanguliza, bali pia kile ulichoacha nyuma. Urithi wako si yale ambayo watu watasema juu yako wakati wa mazishi yako, bali ni yale yatakayoendelea kukunufaisha au kukudhuru hata baada ya kuzikwa.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema na amani zimshukie) ametupa kanuni inayoweka wazi jambo hili: “Mwanadamu anapokufa, amali zake zote hukatika isipokuwa mambo matatu: sadaka yenye kuendelea, elimu yenye manufaa, au mtoto mwema anayemuomba.” [Sahih Muslim, hadith namba 1631]. Ni mambo hayo matatu tu; si mali, si hadhi wala vyeo!

Swali hili huenda lisifurahishe, lakini ni muhimu: Umesambaza elimu gani ambayo itaendelea kuwa na manufaa hata baada ya kifo chako? Umeanzisha wema gani ambao

utaendelea kuzaa matunda hata baada ya wewe kuondoka? Umemlea nani ambaye ataendelea kukukumbuka katika dua zake, hata wakati ulimwengu utakapokuwa umesahau jina lako?

Ndugu zangu katika imani, waja wema waliotangulia walilielewa jambo hili kwa undani. Hawakuishi duniani kwa ajili ya matukio ya muda mfupi, bali waliishi kwa ajili ya kuacha urithi wa kheri na mwendelezo wa amali zao njema.

Mtu alimfundisha mwanafunzi wake kwa dhati akitumaini kwamba Siku ya Hukumu, mwanafunzi huyo atakuwa sehemu ya nuru yake.

Mwanamke alimlea mtoto wake kwa kuzingatia tauhidi akitumaini kwamba kila sijda ya mtoto huyo ingeongeza thawabu katika mizani ya mema yake.

Waja wema waliotangulia waliwekeza katika mambo yasiyoweza kuoza. Lakini leo, watu wengi wanawekeza zaidi katika mambo yanayokwisha haraka. Muda mwingi hupotezwa katika mambo yasiyo na maana, huku miaka mingi iki-tumika kujenga vitu ambavyo havitaambatana nao hadi makaburini, achilia mbali maisha ya baada ya hapo.

Mwenyezi Mungu anasema: “...na mema yanayobakia ni bora mbele ya Mola wako kwa thawabu na matumaini mema zaidi.” [Qur’an, 18:46]. Matendo mema yanayodumu ndiyo mtaji wako halisi. Si kile kinachopita kwa muda mfupi, bali kile kinachobaki hata baada ya wewe kuondoka duniani.

Kwa hiyo, jenga urithi wako kwa kuzingatia mambo haya: Fundisha hata aya moja kwa usahihi, fafanua hadith moja kwa uadilifu na muongoze hata mtu mmoja kumwelekea Allah ‘Azza wa Jallah’.

Toa sadaka yenye kuendelea hata ikiwa ni kidogo, mradi iwe na manufaa ya kudumu. Lea, shauri na waongoze wengine katika haki, kwa sababu athari ya wema inaweza kuendelea kwa vizazi vingi.

Ndugu zangu katika imani, msipuuzi athari ya kudumu ya wema. Neno moja unalolisema leo linaweza kumuongoza mtu ambaye hueda usiwahi kukutana naye. Mtu huyo anaweza kuwaongoza mamia ya wengine, na manufaa ya yote hayo yakakurudia hata wakati utakapokuwa umelala chini ya ardhi.

Hivyo ndivyo waja wema waliotangulia walivyoacha alama ya kudumu; si kupitia miili yao, bali kupitia urithi waliouacha duniani. Ndugu zangu, tunche Mwenyezi Mungu kwa dhati na tutambue kwamba urithi haujengwi mwishoni mwa maisha yetu.

Unajengwa kupitia machaguo tunayofanya kila siku, mara nyingi bila hata kutambua. Urithi hujengwa unapochagua uaminifu badala ya kujionesha, subira badala ya kujibu kwa hasira, na Akhera badala ya starehe za dunia.

Watu wengi hudhani kwamba wanahitaji jambo kubwa sana ili waache urithi nyuma yao. Lakini ukweli ni tofauti kabisa. Mwendelezo wa matendo mema madogo yanayofanywa kwa dhati unaweza kujenga urithi mkubwa.

Njia ya jamii kujikomboa kiuchumi: Kumtanguliza Allah, bidii na kuinuana

Moja ya changamoto kubwa zinazozikabili jamii zetu ni umaskini. Si umaskini wa fedha pekee, bali pia ukosefu wa fursa, ajira, mitaji, maarifa ya biashara na mifumo ya kuinuana. Kuna vijana wenye nguvu lakini hawajui waanzie wapi. Kuna familia zinazofanya kazi kwa bidii lakini hazisongi. Kuna biashara ndogo zinazozaliwa kila mwaka na kufa kabla hazijakomaa.

Katika mazingira kama haya, kila wazo linaloweza kutusaidia kufikiri upya namna tunavyojijenga kiuchumi linafaa kutafakariwa.

Wiki hii nilipita mtandaoni nika-kutana na maoni ya kijana mmoja wa Kisomali anayejulikana kama Magical Moha. Alikuwa akieleza sababu tano ambazo, kwa mtazamo wake, zinasaidia kueleza kwa nini Wasomali wengi wameweza kujenga biashara na mitandao ya kiuchumi katika sehemu mbalimbali duniani.

Ni muhimu kusema mapema: haya ni maoni yake, si utafiti wa kisayansi kuhusu Wasomali wote. Lakini wakati mwingine wazo halihitaji kuwa utafiti wa kitaaluma ili litulazimishe kujiuliza maswali ya maana. Na nilipozisoma hoja zake, nikajiuliza: je, huu unaweza kuwa mwanzo wa ramani ya mafanikio kwa jamii zetu ndogo za Kiislamu?

Mungu mbele, juhudi baada yake

Hoja yake ya kwanza ni kuweka uhusiano na Muumba mbele. Anatoa mfano wa mfanyabiashara anayefunga biashara wakati wa Swala na kwenda msikitini. Kwa lugha nyingine, biashara

ni muhimu, lakini si muhimu kuliko Allah.

Hili linafundisha jambo kubwa zaidi kuliko Swala yenyewe: mali isiwe mungu mwingine wa maisha yetu.

Muislamu anafanya kazi, anapanga, anawekeza na anatafuta faida, lakini anajua kuwa riziki iko mikononi mwa Allah. Huo ni mtazamo unaoweza kumpa mtu utulivu wakati biashara inapoyumba na unyenyekevu inapofanikiwa.

Imani, hata hivyo, isiwe kisingizio cha kuto-panga. Tawakkul si kukaa bila kufanya juhudi.

Hakuna mafanikio bila kazi

Hoja ya pili ni kazi kwa bidii. Tuna tabia ya kuona matokeo bila kuona historia yake. Tunaona duka kubwa, hatuoni miaka ya kuanza na meza ndogo. Tunaona kampuni, hatuoni kukataliwa, madeni, hasara na siku ambazo mwenye biashara hakujua kama atafungua kesho.

Mafanikio mengi hayana siri kubwa sana. Yanahitaji mtu kukubali kufanya kazi ambayo wengine wamechoka kuifanya na kuendelea pale ambapo wengine wamesimama.

Lakini hapa pia tunapaswa kuongeza jambo: bidii peke yake haitoshi. Unaweza kufanya kazi sana katika biashara isiyo na soko, kwa njia isiyo na tija au bila maarifa yanayokuwezesha kukua. Tunahitaji bidii yenye maarifa.

Uaminifu ni mtaji unaotembea

Hoja ya tatu ya Magical Moha ni uaminifu. Katika biashara, unaweza kupata fedha kwa hila leo, lakini ukapoteza soko la miaka kumi.

Mteja anapojua kuwa bei yako inaeleweka, bidhaa yako ni ya kiwango ulichoahidi na ukisema “kesho” kweli ni kesho, anaanza kukuamini. Uaminifu hauandikwi kwenye mizania ya biashara, lakini wakati mwingine ndiyo mali kubwa kuliko bidhaa iliyopo dukani.

Kwa jamii ya Kiislamu, hili halipaswi kuwa jambo la ziada. Linapaswa kuwa sehemu ya utambulisho wetu wa biashara.

“Nikipanda, nikuvute na wewe”

Hoja yake ya nne ndiyo iliyonigusa zaidi: kuinuana. Mtu akifanikiwa, asione wengine kama washindani wa kuogopwa tu. Awaze nani anaweza kumfundisha, kumuunganisha, kum-

pa kazi, kumpa taarifa ya fursa au kumsaidia kuanza.

Hapa ndipo jamii inaweza kutoka kwenye mafanikio ya mtu mmoja kwenda kwenye mafanikio ya wengi.

Tungekuwa na biashara kumi zenye mafanikio na kila moja ikamleakijana mmoja au wawili, ikafundisha biashara, ikaunganisha watu na masoko au ikasaidia mwanzo wa biashara nyingine, baada ya miaka michache tungekuwa tumejenga mfumo, si hadithi ya mtu mmoja. Jamii ndogo za Kiislamu zinahitaji kufikiria kwa namna hiyo.

Uwezo wa kuanza tena

Hoja ya tano ni ustahimilivu. Historia ya Wasomali imejaa vipindi vigumu vya vita, kuhama makazi na kuanza maisha katika mazingira mapya. Magical Moha anaona uzoefu huo ukiwa umejenga kwa baadhi yao uwezo wa kusema: tumepoteza, lakini tutaanza tena.

Hilo ni somo muhimu.

Hasara si mwisho wa biashara. Kufeli mradi mmoja si mwisho wa maisha. Wala kukosa fursa leo hakumaanishi hakuna kesho.

Jamii inayojenga uwezo wa kuamka baada ya kuanguka huwa na nguvu kubwa kuliko ile inayotarajia kutokumbana na matatizo.

Lakini kuna kitu kinachokosekana

Hapa ndipo tunapaswa kuyahoji maoni haya, si kuyapokea kama yalivyo. Imani, kazi, uaminifu, kusaidiana na ustahimilivu ni msingi mzuri. Lakini havitoshi peke yake.

Tunapaswa kuongeza maarifa, elimu ya biashara, akiba na uwekezaji, nidhamu ya fedha, uongozi mzuri wa taasisi na mifumo rasmi ya kusaidiana.

Hatupaswi kutegemea kwamba mfanyabiashara aliyefanikiwa atakumbuka kuwasaidia wengine. Tunaweza kujenga mifuko ya uwekezaji, vikundi vya biashara, mifumo ya ulezi, mafunzo ya vijana, ushirika na mitandao ya kuunganisha wenye mitaji na wenye mawazo.

Kwa maneno mengine, tunahitaji kugeuza tabia nzuri kuwa taasisi. Hapo ndipo mawazo ya Magical Moha yanakuwa zaidi ya simulizi kuhusu Wasomali.

SEHEMU YA

2

Dalili za kudhoofika Imani

Magonjwa mengi ya mwili hayaanizi kwa ghafla. Kabla hali haijawa kubwa, mwili hutuma ishara: uchovu, maumivu, homa au mabadiliko ya kawaida ya mwili. Moyo nao una ishara zake. Imani inapodhoofika, mara nyingi mabadiliko huanza kuonekana katika ibada, tabia, namna ya kufikiri na namna mtu anavyoyatazama maisha. Udhaifu wa Imani haumaanishi moja kwa moja kuwa mtu ameondoka katika dini. Muumini anaweza kupitia vipindi vya nguvu na udhaifu. Hatari huanza pale hali ya udhaifu inapogeuka kuwa kawaida na mtu haoni tena haja ya kujirekebisha.

Swala inapoteza uzito wake

Dalili mojawapo ni Swala kuanza kuwa mzigo. Mtu anaswali, lakini mara nyingi kwa haraka, anaichelewesha bila sababu au akili yake huwa mbali kabisa na anachokifanya. Kwa wanaume, Swala ya jama'a inaweza kuanza kuonekana kama jambo la hiari lisilo na umuhimu mkubwa.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alifananiisha Swala tano na mto uliopo mlangoni mwa mtu ambao huoga humo mara tano kwa siku, akieleza namna Swala inavyofuta madhambi [Muslim].

Si kila ukosefu wa khushuu una maana ya Imani dhaifu, lakini hali ya kudumu ya kuto-sumbuliwa na Swala ni ishara ya kujichunguza.

Qur'an inapokuwa mbali na moyo

Mtu anaweza kutumia muda mwingi katika habari, simu, biashara na mazungumzo, lakini siku au wiki zikapita bila kufungua Qur'an kwa mazingatio. Allah Anasema kuhusu Waumini kuwa wanaposomewa Aya Zake "huwazidishia Imani" [Qur'an, 8:2]. Ikiwa Qur'an ni chanzo cha kuongezeka kwa Imani, basi kukaa mbali nayo kunamnyima moyo chanzo muhimu cha nguvu.

Tatizo hapa si idadi ya kurasa pekee. Mtu anaweza kusoma lakini asitafakari. Dalili ya udhaifu inaweza pia kuwa pale Aya hazimsimui tena, hazimfanyi ajitazame wala kubadilisha mwenendo wake.

Dhambi inapoteza uzito

Muumini anaweza kukosea, kwa sababu mwanadamu si mkamilifu. Lakini kuna tofauti

Imani inavyokua, inavyodhoofika na jinsi ya kuiimarisha



kati ya mwenye kukosea kisha akajuta na mwenye kuzoea dhambi mpaka asiione tena kuwa tatizo.

Allah Anasema: "Hakika Allah anawapenda wanaotubu" [Qur'an, 2:222].

Moyo ulio hai huhisi maumivu baada ya kosa. Unapofikia hatua ambayo uongo, kusengeny, kutazama haramu au kuchezea haki za watu havimsumbui tena mtu, hiyo ni ishara nzito zaidi kuliko kosa lenyewe.

Mema yanapoahirishwa bila mwisho

Udhaifu wa Imani unaweza kuonekana pale kila jambo jema linaposogezwa mbele. Kusoma Qur'an ni kesho, kuhudhuria darsa ni wiki ijayo, kurekebisha Swala ni Ramadhani ijayo.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema matendo yanayopendwa zaidi na Allah ni yale yanayodumu, hata kama ni machache [Bukhari; Muslim]. Mtu anayesubiri kila mara "wakati mzuri" wa kufanya mema anaweza kujikuta miaka imepita bila mabadiliko.

Moyo unapokuwa mgumu kwa nasaha

Dalili nyingine ni mtu kutopenda kukumbushwa. Anaposhauriwa kuhusu Swala, tabia au dhambi, badala ya kutafakari anaudhika au anaanza kutafuta makosa ya anayemnasihi.

Moyo wenye Imani haupendi kila nasaha, lakini una uwezo wa kujiuliza: je, katika maneno haya kuna ukweli unaonihusu? Mtu akifikia hatua ya kukataa kila ukumbusho kwa sababu tu unagusa udhaifu wake, hilo linahitaji tahadhari.

Dunia inapokuwa kubwa kuliko Akhera

Hakuna ubaya katika kutafuta riziki, maendeleo au maisha mazuri. Tatizo linatokea pale fedha, kazi, biashara, nyumba, hadhi na starehe vinapotawala fikra kiasi cha Akhera kusahaulika. Allah Anatukumbusha kuwa mafanikio ya mwisho ni kuokolewa na Moto na kuingizwa Peponi [Qur'an, 3:185].

Muumini anapojikuta anaweza kupanga miaka ya maisha ya dunia lakini hafikirii kabisa namna atakavyokutana na Allah, mizani ya moyo imeanza kuyumba.

Dhikri na elimu vinapopotea

Allah Anasema: "Hakika kwa kumkumbuka Allah nyoyo hutulia" [Qur'an, 13:28].

Ulimi unaweza kuwa bize siku nzima, lakini ukawa haumpi Allah nafasi. Vivyo hivyo, mtu anaweza kupoteza hamu ya kusoma Aqida, Hadith, Sira au Fiqh. Elimu ya dini inapogeuka kuwa jambo lisilo na nafasi kabisa katika maisha, Imani hukosa sehemu muhimu ya lishe yake.

Suhaib Ar-Rumi: Aliacha mali, akachagua Hijra

Baada ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) kuwaamuru Maswahaba wake kuhama kutoka Makka kwenda Madina, Suhaib bin Sinan Ar-Rumi (Allah amridhie) aliazimia kutekeleza amri hiyo.

Hata hivyo, Makureish walimzuia na kuweka watu wa kumfuatilia ili kuhakikisha kuwa haondoki Makka.

Suhaib alitafuta mbinu ya kutoroka, lakini walimkamata njiani na kumwambia: “Ewe Suhaib, hatutakuacha uondoke na nafsi yako pamoja na mali yako. Ulikuwa katika mji wa Makka ukiwa fukara, kisha ukatajirika hapa.”

Suhaib akawauliza: “Mnaonaje nikiacha mali yangu yote? Je, mtaniacha niende?” Wakamjibu: “Ndiyo.” Baada ya hapo, wakachukua mali yake yote na kumwacha

aendeleo na safari yake ya Hijra. Suhaib alipofika Quba, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alimfuata na kumpa habari njema kwa kumwambia: “Biashara yako imekuwa na faida, ewe Abu Yahya.” [Twabaqaat ibn Sa’ad].

Mafundisho ya tukio

Tukio hili linatupa mfano wa kujitoa kwa ajili ya dini ya Allah na kufadhilisha radhi zake kuliko maslahi ya dunia. Suhaib alifika Makka akiwa fukara, akajishughulisha na biashara na baadaye Allah akamneemesha kwa mali nyingi na maisha mazuri.

Hata hivyo, hakufungwa na neema hizo kiasi cha kusahau lengo lake la kumridhisha Allah. Alipofanya uamuzi wa kuhama Makka kwenda Madina, Makureish walimzuia na kumtaka aache mali yake yote ili wamruhusu kuondoka.

Bila kusita, Suhaib alikubali. Aliwaachia mali yake yote na kuendelea na safari ya Hijra ili aungane na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie). Alipofika Quba, Mtume alimpokea kwa furaha na kumpa bishara njema, akamwambia: “Biashara yako imekuwa na faida, ewe Abu Yahya.” Mtume alirudia kauli hiyo mara tatu.

Kutokana na msimamo huu wa kiimani aliyouonesha Suhaib

Ar-Rumi, Allah akateremsha aya ambazo zitakuwa zikisomwa siku zote, ikiwa ni sifa na tukio la kuigwa lililofanywa na Swahaba huyu Mtukufu (Allah awe radhi naye): “Na

miongoni mwa watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake.” [Qur’an, 2:207].

Kundi la Maswahaba, akiwemo Ibn Abbas, Anas, Ikrimah na Sa’id bin Musayyib lime-sema kuwa, aya hii iliteremka kwa Suhaib bin Sinan Ar-Rumi baada ya kusilimu katika mji wa Makka na kutaka kuhama, lakini Makureish wakamzuia kuhama yeye pamoja na mali yake, akajikomboa kwa kuwapa mali yake. [Tafsiri ya Qur’an ya Ibn Kathir].

Tukio hili linaonesha uimara wa imani, uthabiti wa msimamo na kujitolea kwa Maswahaba wa Mtume (Allah awaridhie wote) katika kuipa dini kipaumbele kuliko maslahi ya dunia. Kwa Suhaib, mali haikuwa muhimu kuliko dini yake.

Alikuwa tayari kuachana na kila alichokipata kwa ajili ya kupata radhi za Allah na kuwa pamoja na Mtume. Kwa mtu aliyewahi kupitia maisha ya dhiki, kuacha mali yote baada ya kupata utajiri si jambo rahisi.

Mara nyingi, mtu anapopata neema baada ya dhiki, hujitahidi kuzilinda ili asirudi tena katika hali yake ya zamani. Lakini Suhaib alionesha kuwa mapenzi ya kweli kwa Allah yanaweza kumbadilisha mtu mtazamo wake kuhusu dunia na maslahi yake.

Miongoni mwa mambo yanayoashiria udhaifu wa imani katika zama hizi ni namna baadhi ya Waislamu wanavyoipa dunia nafasi kubwa kuliko dini. Badala ya kutumia mali zao kuihudumia dini na kuwasaidia wenye uhitaji, baadhi yao huitumia dini kama njia ya kujipatia maslahi binafsi.

Wakati mwingine wanachukua hata mali za Waislamu ambazo watu walizitoa wakfu kwa ajili ya kuihudumia dini na kuziuzia ili kupata fedha kwa ajili ya kutatua shida zao.

Hapa ndipo tunapopaswa kutafakari kwa kina kisa cha Suhaib. Yeye aliacha mali yake yote kwa ajili ya dini na akatanguliza radhi za Allah mbele ya maslahi ya dunia. Nasi tuna nafasi ya kufanya “biashara” yenye faida kama ya Suhaib kwa kutumia mali, muda na uwezo tuliopewa na Allah katika mambo ya kheri.

Njia za kutoa katika kheri ni nyingi, na Qur’an pamoja na Sunna zimetufundisha maeneo mbalimbali ya kutumia mali zetu kwa ajili ya Allah. Uzito wa kisa cha Suhaib haupo tu katika wingi wa mali aliyoiacha, bali zaidi katika nia yake, uimara wa imani yake na utayari wake wa kutanguliza radhi za Allah mbele ya maslahi ya dunia.

Dalili 9 kuwa taasisi ina utamaduni mzuri wa kazi

Kwa nini baadhi ya taasisi zina wafanyakazi wenye ari, wabunifu na wanaojituma, wakati nyingine zinakabiliwa na migogoro, malalamiko na wafanyakazi wanaotamani kuondoka? Mara nyingi, tofauti haipo katika mishahara au ukubwa wa taasisi pekee, bali katika utamaduni wa kazi unaojengwa na viongozi pamoja na wafanyakazi.

Utamaduni wa kazi ni mkusanyiko wa maadili, tabia, mitazamo na namna watu wanavyoshirikiana katika taasisi. Unajidhihirisha kupitia jinsi viongozi wanavyowatendea wafanyakazi, namna maamuzi yanavyofanyika na jinsi mafanikio au makosa yanavyoshughulikiwa.

Taasisi zinaweza kuwa na sera nzuri zilizoandikwa, lakini ikiwa wafanyakazi wanaogopa kutoa maoni, hawathaminiwi au wanapandishwa vyeo kwa upendeleo, ni vigumu kusema ina utamaduni mzuri wa kazi. Mtaalamu wa masuala ya uongozi, Justin Wright, ametaja viashiria tisa vinavyoweza kutumiwa kupima afya ya utamaduni wa taasisi.

Kwanza, wafanyakazi wanapaswa kujisikia kwamba wanasikilizwa na kuthaminiwa. Mfanyakazi anayetoa pendekezo na kuona linafikiwa kwa uzito huwa na sababu zaidi ya kujihusisha na maendeleo ya taasisi.

Hata hivyo, kusikiliza pekee hakutoshi. Viongozi wanapaswa kuchukua hatua kuhusu changamoto zinazowasilishwa, badala ya kukusanya maoni ambayo hayafanyiwi kazi.

Pili, utamaduni mzuri unajengwa katika kuaminiana na kuheshimiana. Kila mfanyakazi, kuanzia mlinzi hadi meneja mkuu, anapaswa kutendewa kwa heshima bila kujali cheo chake.

Heshima haimaanishi kukubaliana katika

kila jambo. Inamaanisha kutambua utu wa mwingine hata pale kunapokuwa na tofauti za kimawazo.

Tatu, wafanyakazi wanapaswa kujisikia salama kuwa wao wenyewe. Katika mazingira hayo, mfanyakazi anaweza kukiri kosa, kuuliza swali au kueleza wasiwasi bila kuogopa kudhalilishwa.

Hali hii huitwa usalama wa kisaikolojia, yaani mazingira yanayomwezesha mtu kuzungumza kwa uwazi bila hofu ya kuadhibiwa au kuibishwa kwa kutoa maoni ya kujenga.

Nne, viongozi wanapaswa kuwasiliana kwa uwazi na uaminifu. Kuficha taarifa muhimu, kutoa ahadi zisizotekelezeka au kubadilisha maamuzi bila maelezo kunadhoofisha uaminifu.

Hata taasisi zinapokabiliwa na changamoto za kifedha, kueleza hali halisi kwa kiwango kinachofaa kunaweza kusaidia wafanyakazi kuelewa kinachoendelea badala ya kutegemea uvumi.

Tano, utamaduni mzuri unawapa wafanyakazi nafasi ya kukua kitaaluma. Mafunzo, ushauri, majukumu mapya na fursa za kujifunza huwasaidia kuongeza uwezo wao.

Mfanyakazi anapoona hana nafasi ya kuendelea, anaweza kupoteza ari hata kama analipwa vizuri.

Sita, wafanyakazi wanapaswa kuheshimu mawazoyawenza nakuyajadilikwahoja. Timu yenye afya si ile inayokubaliana kila wakati, bali inayoweza kutofautiana bila kugombana.

Kwa mfano, mfanyakazi mdogo anaweza kuwa na pendekezo bora kuliko meneja wake. Utamaduni mzuri unaruhusu pendekezo hilo kusikilizwa na kupimwa kwa ubora wake.

Saba, taasisi haipaswi kuvumilia

tabia zinazoharibu mazingira ya kazi. Vitisho, matusi, unyanyasaji, ubaguzi na matumizi mabaya ya madaraka vinapaswa kushughulikiwa kwa haki na uthabiti.

Hata mfanyakazi anayezalisha faida kubwa hapaswi kupewa kinga ya kuwadhalilisha wengine kwa sababu ya mafanikio yake.

Nane, kupandishwa cheo kunapaswa kutegemea uwezo, utendaji na sifa zinazohitajika, badala ya undugu, urafiki au upendeleo wa viongozi.

Wafanyakazi wanapoona juhudi na uwezo vinathaminiwa, wanapata motisha ya kufanya vizuri zaidi.

Tisa, mawazo bora yanapaswa kupewa nafasi bila kujali yametoka kwa nani. Taasisi inayosikiliza viongozi pekee inaweza kupoteza ubunifu unaotokana na wafanyakazi walioko karibu zaidi na wateja na changamoto za kila siku. Katika mtazamo wa Kiislamu, misingi hii inaendana na maadili ya uadilifu, uaminifu, mashauriano na kuheshimu haki za wengine.

Allah anaamrisha kutekeleza amana na kuhukumu baina ya watu kwa uadilifu [Qur'an, 4:58]. Kanuni hiyo inawahusu pia viongozi wenye dhamana ya kusimamia wafanyakazi.

Hata hivyo, utamaduni mzuri haujengwi kwa hotuba za viongozi au maandishi yanayobandikwa ukutani pekee. Unajengwa kupitia maamuzi ya kila siku: nani anasikilizwa, nani anathaminiwa, nani anapewa nafasi na tabia zipi hazivumiliwi.

Viongozi wanaotaka kuboresha mazingira ya kazi wanaweza kuanza kwa kuwauliza wafanyakazi kinachowazuia kufanya kazi kwa ufansi, kutambua michango yao, kuruhusu mawazo tofauti, kushughulikia tabia mbaya na kuwekeza katika maendeleo yao.

Hatimaye, utamaduni mzuri wa taasisi haupimwi kwa jinsi viongozi wanavyozungumzia, bali kwa namna wafanyakazi wanavyoishi kila siku. Taasisi zinayowaheshimu watu wake inajiwekea msingi imara wa ushirikiano, ubunifu na mafanikio ya kudu-mu.



Mwanao anajisikia huru kukueleza anayoyapitia?

Wazazi wengi hutumia nguvu kubwa kuhakikisha watoto wao wanakuwa na nidhamu, wanaheshimu wakubwa, wanaswali na kufuata maadili ya dini. Hata hivyo, katika juhudi hizo, baadhi yao husahau jambo muhimu katika malezi: kujenga uhusiano wa karibu unaomfanya mtoto ajisikie kupendwa, kuthaminiwa na kuwa huru kueleza yanayomsumbua.

Fikiria mama mwenye mtoto wa miaka 15 anayefanya kila anachoagizwa. Anaswali, anaheshimu wazazi na hana matatizo ya nidhamu shuleni. Kwa nje, anaonekana kuwa mtoto mwenye malezi mazuri.

Lakini mama huyo anapojaribu kuzungumza naye kuhusu maisha yake, marafiki au mambo yanayomhangaisha, hapati majibu zaidi ya “sijui”, “hakuna kitu” au “niko sawa”.

Anaishi na mtoto wake katika nyumba moja, lakini hajui kinachoendelea moyoni mwake. Hali hii inaweza kuwakumba hata wazazi wanaojitahidi kutekeleza wajibu wao. Mtoto anaweza kuwa mtiifu lakini asiwe na ukaribu wa kihisia na wazazi wake.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), kujenga uhusiano mzuri na mtoto wa umri wa balehe ni msingi muhimu wa kumsaidia kukabiliana na changamoto za kihisia na kijamii.

Mzazi anawezaje kujenga ukaribu na

mtoto?

Kwanza, tenga muda wa kuwa na mtoto wako. Uhusiano wa karibu haujengwi kwa maelekezo pekee, bali kwa muda mnaotumia pamoja. Si lazima kumpeleka katika matembezi ya gharama kubwa. Mnaweza kutembea, kupika, kufanya shughuli za nyumbani au kuzungumza mkiwa safarini.

Mwandishi wa masuala ya malezi, Zakeeya Ali, anashauri wazazi kutenga muda maalumu wa kuwa na watoto wao, wakishiriki shughuli wanazozipenda.

Pili, msikilize zaidi kuliko unavyomfundisha. Mtoto anapoanza kueleza tatizo, usikimbilie kumkatiza kwa mawaidha au kumweleza alichokosea. Badala yake, muulize: “Unaweza kunieleza zaidi?” au “Unadhani tufanye nini kuhusu jambo hilo?”

UNICEF inashauri wazazi kutumia maswali yanayomruhusu mtoto kujieleza na kuonyesha kwamba wanazingatia anachosema. Wakati mwingine mtoto hahitaji suluhisho la haraka. Anahitaji mtu wa kumsikiliza bila kumhukumu.

Tatu, usifanye kila mazungumzo kuwa mahojiano. Ikiwa kila unapokutana na mtoto unauliza kuhusu masomo, kazi za nyumbani, swala au makosa aliyofanya, anaweza kuanza kuyaepuka mazungumzo hayo.

Zungumzieni pia mambo anayoyapenda, marafiki, michezo na matukio yanayomfurahisha. Muulize maoni yake kuhusu mambo mbalimbali. Mazungumzo ya kawaida yanaweza kujenga uaminifu unaomsaidia mtoto kukueleza matatizo makubwa baadaye.

Nne, tambua na uheshimu hisia zake. Mtoto anapokasirika au kuhuzunika, usimwambie kwamba anachohisi ni upuuzi. Unaweza kusema: “Naona jambo hili limekuumiza. Ungependa tulizungumzie?”

Hii haimaanishi kwamba unakubaliana na kila anachosema, bali unatambua kwamba hisia zake zina umuhimu.

Tano, dhibiti hasira anapokueleza jambo linalokushtua. Mtoto anaweza kukiri kwamba amefanya kosa kubwa au amekumbwa na tatizo shuleni.

Mzazi anayejibu kwa kufoka, vitisho au kumdhalilisha anaweza kumfanya mtoto

aogope kusema ukweli wakati mwingine. Ni bora kumsikiliza kwanza, kuelewa kili-chotokea na kisha kumwelekeza kwa utulivu, huku akiendelea kuwajibishwa kwa makosa yake.

Sita, onyesha upendo kwa vitendo. Mpongeze mtoto anapofanya jambo zuri, mtayarishie chakula anachokipenda au mtumie ujumbe mfupi wa kumtia moyo.

Kwa baadhi ya watoto, kukumbatiwa ni faraja kubwa; wengine hupendelea kuonyeshwa upendo kwa maneno au muda wa pamoja. Zingatia namna mtoto wako anavyojisikia vizuri.

Saba, kubali unapokosea na uwe mfanomwema. Ikiwa ulimfokea bila sababu, mwambie: “Nilikosea kuzungumza nawe kwa hasira. Samahani.”

Kukiri kosa hakupunguzi heshima ya mzazi. Kunamfundisha mtoto unyenyekevu, uwajibikaji na namna ya kurekebisha mahusiano. Vilevile, usimfundishe tabia ambazo wewe mwenyewe huzitekelezi. Watoto hujifunza mengi kutokana na matendo ya wazazi kuliko maelekezo yao.

Nane, usimlazimishe kuzungumza kila wakati. Watoto wa umri wa balehe huhitaji pia faragha na nafasi ya kujitegemea.

Mtoto asipotaka kuzungumza wakati fulani, mhakikishie kwamba uko tayari kumsikiliza atakapohitaji. Wakati mwingine, hata kukaa pamoja bila mazungumzo mengi hujenga ukaribu.

Katika Uislamu, malezi yanapaswa kuambatana na upendo, huruma na mfanomwema. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa akionyesha mapenzi kwa watoto na kuisitiza umuhimu wa kuwahurumia wengine [Bukhari, 5997].

Hivyo, kujenga ukaribu na mtoto hakuamaanishi kuacha nidhamu, maelekezo au kumfundisha dini. Badala yake, uhusiano wa kuaminiana unaweza kumsaidia kupokea nasaha kwa moyo ulio wazi.

Hatimaye, mzazi anapaswa kujiuliza: Je, mtoto wangu akikabiliwa na tatizo kubwa au kufanya kosa linalomtisha, atakuwa tayari kunieleza, au atafanya kila awezalo kuhakikisha silijui?

Jibu la swali hilo linaweza kueleza mengi kuhusu ubora wa uhusiano kati yao.

Mtoto hahitaji mzazi anayemwekea sheria pekee. Anahitaji pia mzazi anayemfanya ajisikie salama kusema ukweli, hata pale ukweli huo unapokuwa mgumu kusikiliza.

Nini kinachowavutia wazazi kupeleka watoto shule za bei ghali?

Kwa nini mzazi akubali kulipa mamilioni ya shilingi kila mwaka kumpeleka mtoto katika shule ya gharama kubwa wakati kuna shule nyingine zenye ada nafuu, au hata zisizotoza ada? Je, anatafuta elimu bora, umahiri wa Kiingereza, hadhi katika jamii au nafasi ya mtoto wake kujenga urafiki na watoto wa familia zenye uwezo? Tafiti zinaonyesha kwamba sababu hizo zinaweza kuchanganyika. Kwa wazazi wengi, elimu ni uwekezaji muhimu hivyo hupunguza matumizi mengine, kukopa au kufanya kazi za ziada ili kuhakikisha watoto wanasoma katika shule bora za binafsi. Hata hivyo, gharama kubwa si uthibitisho wa moja kwa moja wa ubora. Wakati mwingine, wazazi hawalipii ufundishaji pekee, bali pia mazingira, lugha, hadhi na fursa zinazohusishwa na jina la shule.

Kiingereza na matarajio ya elimu bora

Moja ya vivutio vikubwa ni lugha ya Kiingereza. Katika jamii nyingi za Afrika, shule zinazofundisha kwa Kiingereza huonekana kuwa na hadhi ya juu na zinazoweza kuwaandaa wanafunzi kwa elimu na ajira za kimataifa.

Nchini Tanzania, mvuto huo umeonekana pia katika shule za serikali zinazofundisha kwa Kiingereza. Gazeti The Citizen, katika makala ya Novemba 2024 kuhusu shule hizo, liliripoti mjadala kuhusu gharama na tofauti za mazingira

gira ya kujifunzia.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, John Kalage, alionya kwamba dhana ya shule zinazofundisha kwa Kiingereza kuwa bora kuliko zinazofundisha kwa Kiswahili inaweza kuongeza matabaka katika elimu, akitoa mfano shule za serikali zinazofundisha kwa Kiingereza zilikuwa na uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 55, ikilinganishwa na mmoja kwa 63 katika shule zinazofundisha kwa Kiswahili.

Hivyo, mvuto wa shule hizo unaweza kutokana pia na mazingira ya kujifunzia, si lugha pekee. Kujua Kiingereza ni ujuzi muhimu, lakini kuna tofauti kati ya kujifunza lugha vizuri na kuelewa masomo yanayofundishwa kwa lugha hiyo.

Hadhi, marafiki na shinikizo la kijamii

Kivutio kingine ni hadhi ya kijamii. Kwa baadhi ya familia, shule anayosomea mtoto inaweza kuwa sehemu ya utambulisho wa kiuchumi na kijamii.

Utafiti wa Pere Ayling na Derron Wallace, uliochapishwa mtandaoni mwaka 2024 katika International Studies in Sociology of Education, ulichunguza sababu zinazowafanya wazazi matajiri nchini Nigeria kuchagua shule za kimataifa.

Matokeo yalionyesha kwamba wazazi waliohusishwa katika utafiti hawakuzingatia sana alama nzuri za mitihani kama kipimo cha ubora. Badala yake, walithamini utaifa na rangi ya walimu pamoja na mbinu za ufundishaji zinazohusishwa na mfumo wa Uingereza.

Watafiti walihitimisha kwamba uchaguzi huo pia ulikuwa njia ya kuimarisha mipaka ya kitabaka. Kwa maana hiyo, shule inaweza kuwa zaidi ya mahali pa kupata elimu; inakuwa pia alama ya hadhi ambapo mtoto hupata nafasi ya kusoma pamoja na watoto wa wafanyabiashara, viongozi au wataalamu wenye ushawishi.

Urafiki huo unaweza kutoa fursa za taarifa, ushauri na mahusiano yenye manufaa baadaye, ingawa hakuna uhakika kwamba kila mwanafunzi atanufaika.

Pia kuna shinikizo la kijamii. Mzazi anaweza kushawishika kuchagua shule kwa sababu watoto wa ndugu au marafiki zake wanasoma huko. Hata hivyo, kiwango ambacho sababu hizi huathiri wazazi wa Tanzania bado kinahi-

taji uchunguzi wa moja kwa moja.

Je, shule binafsi zina ubora wa kweli?

Utafiti wa Kasper Brandt, uliochapishwa mwaka 2023 katika jarida la Economic Development and Cultural Change, ulichambua rekodi za mitihani za wanafunzi 635,000 nchini Tanzania.

Ulibaini kwamba shule binafsi za sekondari zilizochunguzwa zilikuwa na faida ya wastani katika matokeo ya mitihani, baada ya kuzingatia uwezo wa awali wa wanafunzi na mambo mengine. Faida hiyo ilikuwa kubwa zaidi katika Hisabati kuliko Kiswahili na Kiingereza.

Huu ni ushahidi kwamba shule binafsi zinaweza kuwa na manufaa halisi ya kitaaluma, si hadhi pekee.

Hata hivyo, utafiti wa Rob Gruijters, Benjamin Alcott na Pauline Rose wa mwaka 2021, uliohusisha Kenya, Uganda, India na Pakistan, ulibaini kwamba faida ya shule binafsi ilipungua kwa takribani nusu katika Kenya na Uganda baada ya kuzingatia tofauti za kifamilia. Kwa hiyo, sehemu ya tofauti za ufaulu inaweza kutokana na mazingira na msaada ambao watoto hupata nyumbani.

Shule binafsi zinaweza pia kuwavutia wazazi kwa madarasa yenye wanafunzi wachache, ufuatiliaji wa karibu, nidhamu, usalama na vifaa vya kujifunzia.

Katika makala ya The Citizen ya Februari 2015, wazazi walieleza kuchagua shule binafsi kutokana na wasiwasi kuhusu ubora wa elimu katika baadhi ya shule za serikali. Hata hivyo, matatizo hayo hayahusu shule zote za serikali, kama ambavyo ubora hauwezi kudhaniwa katika kila shule binafsi.

Aidha, makala ya maoni iliyochapishwa na The Citizen Desemba 2015 iliibua malalamiko kuhusu ada kubwa na michango ambayo baadhi ya wazazi walidai haiendani na huduma zinazotolewa. Kwa hiyo, kabla ya kuchagua shule, mzazi anapaswa kuchunguza ubora wa walimu, matokeo ya wanafunzi, nidhamu, usalama na namna shule inavyomsaidia kila mtoto kujifunza.

Ni muhimu pia kupima gharama dhidi ya uwezo wa familia. Elimu ya mtoto mmoja haipaswi kuifanya familia ishindwe kutimiza mahitaji mengine muhimu.

Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA

6

Tumia AI kuiandaa habari kwa majukwaa tofauti

Zamani habari ingeandikwa kwa gazeti, redio au televisheni na kazi ikaonekana imekamilika. Leo habari moja inaweza kuhitajika kwenye tovuti, mitandao ya kijamii, WhatsApp, jarida la barua pepe, video fupi au hata sauti.

Hapa kuna kazi nyingine kubwa kwa mwandishi na chumba cha habari: Habari ile ile iwasilishwe kwa namna inayofaa kila jukwaa bila kubadilisha ukweli wake. AI inaweza kusaidia sana katika hatua hii.

Habari moja haiwasilishwi sawa kila mahali

Habari ya maneno 800 inayofaa kwenye tovuti haiwezi kuwekwa yote kwenye ujumbe wa WhatsApp. Vivyo hivyo, kichwa cha habari cha gazeti si lazima kifae moja kwa moja kama maelezo ya video ya sekunde 30.

Hivyo, habari inaweza kuhitaji kufupishwa, kupewa kichwa tofauti au kubadilishwa namna ya kuwasilishwa kulingana na jukwaa. AI inaweza kusaidia kufanya mabadiliko hayo kwa haraka.

Kwa mfano, baada ya habari kuhaririwa na kuthibitishwa, mwandishi anaweza kuiomba AI itengeneze muhtasari mfupi wa WhatsApp, ujumbe wa mitandao ya kijamii au maandishi ya sauti ya dakika moja. Hii inaweza kupunguza



kazi ya kurudia kuandika jambo lilelile mara nyingi.

Kilichobadilika ni namna ya kuwasilisha, si ukweli

Hii ndiyo kanuni muhimu zaidi.

Makala inaweza kuwa ndefu kwenye tovuti na fupi kwenye WhatsApp. Video inaweza kutumia sentensi chache zaidi. Kichwa cha mitandao ya kijamii kinaweza kuwa tofauti na cha gazeti.

Lakini takwimu, majina, nukuu na maana ya habari haviwezi kubadilishwa ili tu bidhaa iwe ya kuvutia zaidi. AI inaweza kuwa na kishawishi cha kufupisha mpaka kuondoa maelezo muhimu. Inaweza pia kutengeneza kichwa kinachovutia sana lakini kikatoa picha tofauti na habari yenyewe. Kwa hiyo, kila toleo jipya lazima lipitiwe na mwandishi.

Kutoka habari kwenda kwenye video au sauti

Habari iliyoandikwa inaweza kuwa msingi wa bidhaa nyingine. AI inaweza kusaidia kutengeneza rasimu ya maandishi ya video fupi au sauti kutokana na habari ambayo tayari imekamilika.

Lakini video nzuri si kusoma makala yote mbele ya kamera. Inahitaji kuchagua jambo kuu, kulieleza kwa lugha inayofaa kusikilizwa na kulipanga kwa muda uliopo.

AI inaweza kusaidia kutoa rasimu ya namna hiyo. Mwandishi anaweza kisha kuifupisha, kui-boresha na kuhakikisha kwamba haijaongeza jambo ambalo halipo kwenye habari ya awali.

Hivyo, badala ya kuanza kila bidhaa kutoka sifuri, newsroom inaweza kutumia habari moja iliyothibitishwa kutengeneza bidhaa kadhaa.

Inaweza kusaidia kuandaa vichwa tofauti

Kila jukwaa lina namna yake ya kuvutia msomaji. Kichwa cha gazeti, tovuti na ujumbe wa mitandao ya kijamii vinaweza kutofautiana, ingawa vinazungumzia habari moja. AI inaweza kutoa mapendekezo kadhaa ya vichwa na mwandishi akachagua kinachofaa. Hilo linaweza kuwa na manufaa hasa pale chumba cha habari kinapohitaji matoleo kadhaa kwa majukwaa tofauti.

Lakini hapa ndipo tahadhari ya “kubofya kwa lazima” inapohitajika. Kichwa kisiahidi jambo ambalo habari haitoi. Kisifanye tahadhari ionekane kama uhakika, wala kisibadilishe ukubwa wa jambo ili kuvutia wasomaji.

Muhtasari unaweza kusaidia msomaji mwenye muda mdogo

Wasomaji hawatumii habari kwa namna moja. Mmoja anaweza kusoma makala yote, mwingine ana dakika moja tu, na mwingine anataka kujua mambo makuu kabla ya kuamua kama asome zaidi.


AI inaweza kusaidia kutengeneza muhtasari mfupi wa habari ndefu. Hii inaweza kutumika kwenye tovuti, WhatsApp au majukwaa mengine.

Lakini muhtasari mzuri unapaswa kuhifadhi maana ya habari. Ukifupisha sana, unaweza kuondoa tahadhari, masharti au upande mwingine wa mjadala na kuacha picha potofu. Kwa hiyo, ufupisho nao ni kazi ya kiuhariri, si ya kimitambo tu.

Habari inaweza pia kujibiwa kwa maswali na majibu

Baadhi ya habari zinaeleweka vizuri zaidi zikibadilishwa kuwa maswali na majibu. Kwa mfano, mabadiliko ya kodi, sera mpya au huduma mpya yanaweza kuwafanya wasomaji waulize: Nani anaathirika? Mabadiliko yanaanza lini? Nitapaswa kufanya nini?

AI inaweza kusaidia kutengeneza rasimu ya maswali hayo kutokana na habari iliyokwisha kuthibitishwa. Hii inaweza kuwa njia nzuri ya kuifanya habari iwe rahisi kueleweka.



Usafi wa kinywa: Mafundisho ya Mtume na ushauri wa wataalamu

Katika Uislamu, usafi wa kinywa umepewa umuhimu mkubwa, hasa kupitia matumizi ya siwak, kijiti kinachotumika kusafisha meno. Mtume amesema kwamba lau isingekuwa kuwapa uzito watu wake, angewaamrisha kutumia siwak kila wanapotaka kuswali [Bukhari].

Hadith nyingine zinaonyesha kwamba Mtume alitumia siwak ali-poamka usiku kwa ajili ya swala na alipokuwa akiingia nyumbani.

Katika tukio lenye kugusa moyo, Aisha (Allah amridhie) amesimulia kwamba hata muda mfupi kabla ya kufariki, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alitumia siwak aliyomuandalia na kumpa [Bukhari]. Mfano huo unaonyesha namna usafi wa kinywa ulivyokuwa sehemu muhimu ya maisha yake.

Watu wengi husafisha meno kila siku, lakini si wote wanaofanya hivyo kwa usahihi. Baadhi hupiga mswaki kwa sekunde chache, wengine hutumia nguvu nyingi, huku wengine wakiamini kwamba kusafisha meno asubuhi pekee kunatosha.

Wataalamu wa afya wanaeleza kwamba muda, mbinu na vifaa vina- vyotumika vina umuhimu mkubwa katika kuzuia meno kuoza, magonjwa ya fizi na harufu mbaya ya kinywa.

Kwa mujibu wa makala ya Harvard Health Publishing ya Oktoba 2, 2026, usafi mzuri wa kinywa husaidia kulin- da meno na fizi, na kumwezesha mtu kutafuna, kuzungumza na kufurahia chakula vizuri hata anapozeeka.

Magonjwa mengi ya kinywa huanza kwa mkusanyiko wa utando mwembamba wenye bakteria unao- itwa plaque. Usipoondolewa, unawe- za kusababisha meno kuoza na fizi kuvimba au kutoa damu. Baadaye unaweza kukakamaa na kuwa tartar, uchafu mgumu unaohitaji kuondole- wa na mtaalamu wa meno.

Lakini ni kwa namna gani mtu anaweza kutunza meno na kinywa



chake kwa usahihi? Yafuatayo ni maelekezo muhimu ya kitaalamu.

Muda na mbinu sahihi za kusafi- sha meno

Kwanza, piga mswaki mara mbili kwa siku. Shirika la Madaktari wa Meno la Marekani (ADA) linashauri kusafisha meno kwa dakika mbili kila unapopiga mswaki.

Wakati unaofaa ni asubuhi na kabla ya kulala usiku. Unaweza kutumia sekunde 30 kusafisha kila robo ya kinywa, ukihakikisha sehemu zote za meno zimefikwa.

Pili, tumia mbinu sahihi. Shikilia mswaki kwa mwelekeo wa nyuzi 45 kuelekea mpaka wa meno na fizi. Sug- ua taratibu kwa mizunguko midogo au misogeo mifupi. Safisha sehemu za nje, ndani na zinazotumika kuta- funia.

Kwa meno ya mbele, shikilia mswa- ki wima ili kusafisha sehemu zake za ndani. Epuka nguvu nyingi zinazowe- za kuumiza fizi na kuchangia ucha- kavu wa meno.

Tatu, chagua mswaki na dawa sahi- hi. Tumia mswaki wenye manyoya laini. Mswaki wa kawaida unawe- za kufanya kazi vizuri, ingawa wa umeme unaweza kurahisisha usafi- shaji. Badilisha mswaki kila baada ya miezi mitatu hadi minne, au mapema

ikiwa manyoya yameharibika.

Dawa ya meno inapaswa kuwa na fluoride (floridi), madini yanayosaid- ia kuimarisha tabaka la nje la meno na kupunguza hatari ya kuoza.

Baada ya kupiga mswaki, tema dawa iliyobaki, lakini usisukutue kwa maji mara moja ili floridi iendelee kulinda meno.

Usisahau nafasi za meno na ulimi

Nne, safisha nafasi kati ya meno. Mswaki hauwezi kufikia vizuri seh- emu zote kati ya meno.

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya ya Meno na Kinywa ya Marekani (NIDCR) inapendekeza kusafisha nafasi hizo kila siku kwa kutumia uzi maalumu (dental floss) au brashi ndogo.

Uzi uzungushwe kwenye ubavu wa jino kwa umbo la herufi C, kisha kusogezwa juu na chini bila kujeruhi fizi. Tano, safisha ulimi. Bakteria na mabaki ya chakula yanaweza kujik- usanya kwenye ulimi na kuchangia harufu mbaya ya kinywa.

Tumia kifaa maalumu au mswaki laini, ukisafisha taratibu kutoka nyu- ma kuelekea mbele.

Sita, tumia dawa ya kusukutua inapohitajika. Dawa za kusuku- tua kinywa (mouthwash) zinaweza kusaidia kupunguza bakteria au kuzuia meno kuoza, kulingana na viambato vyake.

Hata hivyo, si mbadala wa mswaki na uzi wa meno. Huduma ya Taifa ya Afya ya Uingereza (NHS) inashauri kuitumia wakati tofauti na kupiga mswaki, kwa mfano baada ya chakula cha mchana.

Kwa wanaotumia siwak, inaweza kusaidia kuondoa utando wa bakteria inapokuwa safi na kutumiwa vizuri. Ni vyema kuitumia kama nyongeza ya mswaki na dawa yenye floridi, si mbadala wake.

Jinsi ya kuwafikishia watoto habari za huzuni kwa hekima na upendo

Kifo cha mzazi, ndugu au mtu wa karibu, ugonjwa hatari, ajali na majanga ni miongoni mwa matukio yanayoweza kuathiri maisha ya mtoto kisaikolojia. Wakati mwingine wazazi huwafikishia watoto habari hizo wakidhani wanawalinda dhidi ya huzuni. Hata hivyo, wataalamu wa saikolojia wanashauri kusema ukweli kwa upole, huku Uislamu ukisisitiza rehema, subira na kumtegemea Allah wakati wa mitihani. Kumweleza mtoto kwamba mama yake amefariki dunia au baba yake ana ugonjwa hatari si jambo rahisi. Hata watu wazima wakati mwingine hukosa maneno ya kuelezea habari zinazoumiza moyo. Hofu huwa ni namna mtoto atakavyopokea taarifa hizo. Je, atalia, atashtuka au atauliza maswali magumu? Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa lengo si kumzuia mtoto kuhuzunika, bali kumsaidia kuelewa kilichotokea na kukabiliana na hali hiyo akiwa katika mazingira yenye upendo na usalama. Kwa familia za Kiislamu, mafundisho ya dini yanaweza kuwa chanzo muhimu cha faraja, lakini yanapaswa kutumiwa kwa hekima kulingana na umri wa mtoto.

Sema ukweli, usimfiche mtoto

Baadhi ya wazazi wanapokabiliwa na msiba huwaambia watoto kwamba marehemu amelala au amesafiri kwenda mbali.

Ingawa kauli hizo hutolewa kwa nia njema, zinaweza kumchanganya mtoto. Anaweza kuelewa

ndeleva kusubiri marehemu arudi au kuogopa kulala akidhani usingizi unaweza kusababisha kifo.

Ni bora kusema kwa upole: “Bibi alikuwa mgonjwa sana, lakini amefariki dunia. Hatutaweza kumuona tena akiwa hai.”

Kisha mtoto anaweza kuelekezwa kwamba kifo ni sehemu ya maisha na kwamba Waislamu wanaamini kila mwanadamu atarejea kwa Allah.

Hapa ndipo inapofaa kumfundisha kauli ya Inna lillahi wa inna ilayhi raji’un, yaani, hakika sisi ni wa Allah na kwake tutarejea, kama inavyoelezwa katika Qur’an, Suratul Baqarah, aya ya 156.

Sikiliza kabla ya kueleza mengi

Mtoto anaposikia habari za msiba anaweza kuwa na maswali ambayo mtu mzima hajayafikiria. Kwa mfano: “Mama akifa nani atanipikia?” au “Je, baba naye atakufa?”

Badala ya kumkemea au kuyapuuza maswali hayo, mzazi anapaswa kumsikiliza na kumjibu kwa utulivu.

Katika makala yake kuhusu malezi ya Kiislamu wakati wa majanga, mwandishi Tasneem Abdul Hakeem anasisitiza umuhimu wa kuwasikiliza watoto kabla ya kuwapatia maelezo.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mfano wa huruma kwa watoto. Katika Hadith iliyopokewa na Bukhari, Mtume alisisitiza kwamba asiyeonyesha rehema hatorehemewa.

Hivyo, mtoto mwenye huzuni anahitaji kusikilizwa, kukumbatiwa na kufarijiwa, si kuamriwa kunyamaza.

ZINGATIA UMRI NA UELEWA WAKE

Watoto wadogo, hasa walio chini ya miaka mitano, wanaweza kushindwa kuelewa kwamba kifo ni cha kudumu. Wanahitaji maelezo mafupi, upendo na kuhakikishiwa usalama ilhali watoto wenye miaka sita hadi tisa huanza kuelewa maana ya kifo, lakini wakati mwingine wanaweza kujilaumu wakidhani wamechangia kilichotokea.

Watoto wakubwa wanaweza kuuliza maswali kuhusu sababu za kifo, maisha baada ya kifo na hatima ya familia.

Majibu yanapaswa kuzingatia umri na kiwango cha uelewa wa kila mtoto, bila kutunga habari au kutoa ahadi zisizokuwa na uhakika.

Mfundishe subira, si kuficha huzuni

Uislamu unafundisha kwamba maisha yana mitihani. Allah anasema katika Suratul Baqarah, aya ya 155, kwamba atawaonja watu kwa hofu, njaa na upungufu wa mali na nafsi, kisha anawabashiria mema wenye subira.

Hata hivyo, kumfundisha mtoto subira hakuamaanishi kumkataza kulia. Mtoto anaweza kulia, kuhuzunika au kumkumbuka marehemu. Hayo ni maumbile ya kibinadamu.

Badala ya kumwambia “Usilie, Muislamu anatakiwa kuwa na subira,” ni vizuri kumwambia: “Najua unamkumbuka mama. Ni kawaida kuhuzunika. Tumuombe Allah amrehemu.”

Vilevile, wazazi wanapaswa kuepuka kumweleza mtoto kwamba kila janga ni adhabu ya Allah. Kauli hiyo inaweza kumfanya amuogope Allah kwa namna inayoongeza hofu badala ya kumjengea imani katika rehema Zake.

Mjengee tawakkul na matumaini

Mtoto aliyepoteza mzazi anaweza kuwa na wasiwasi kuhusu maisha yake ya baadaye. Ni muhimu kumweleza nani atakayemtunza, atakapoishi na namna mahitaji yake yatakaavyoshughulikiwa.

Pamoja na faraja hizo, anaweza kufundishwa tawakkul, yaani kumtegemea Allah huku familia ikichukua hatua zinazohitajika kumlinda na kumtunza.

Kwa watoto wanaosikia habari za majanga, wazazi wanaweza kuwahamasisha kuwaombea waathirika au kuwasaidia wenye mahitaji. Hatua hizo huwafundisha kwamba imani haiishii katika kukubali mitihani, bali inahusisha pia kuwafariji na kuwasaidia wengine.

Usimwache mtoto peke yake

Baada ya kufikisha habari za huzuni, jukumu la mzazi au mlezi haliishii hapo. Mtoto anaweza kuonekana mwenye furaha leo, lakini kesho akawa na huzuni kubwa. Wengine wanaweza kubadilika kitabia, kupata matatizo ya usingizi au kushindwa kuzingatia masomo.